**Mbaroni** madai ya kumuua 'shamba boi', mwili wake kuufukia

UKURASA 3



**Adaiwa** kujinyonga baada ya kubainika na maradhi ya UTI

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe

Alhamisi Agosti 5, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580663

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Waziri wa Marekani kuteta na CHADEMA

**LENGO** kujua kinachomsibu Mbowe, Rais Samia ampa ujumbe kuwapelekea... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani anayeshughulikia mambo ya siasa, Balozi Victoria Nuland, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## MBATIA, ZITTO WAMTEMBELEA MBOWE GEREZA KUU UKONGA

UKURASA 2



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro (kushoto), akifanya mazoezi ya pamoja na askari wake jana, wakijiandaa kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini humo leo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 4

## KIONGOZI CCM MBARONI TUHUMA ZA KUUZA ARDHI

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Picha ya Ndege, Kibaha Mjini, Godfrey Mwaipopo, ametiwa mbaroni kwa tuhuma za kuhusika kuuza ardhi kinyume cha taratibu na kusababisha migogoro katika eneo la Lulanzi. Kukamatwa kwa mwenyekiti huyo ni maagizo ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge...



UKURASA WA 7

## RC AONYA WATAKAOUZA CHANJO YA CORONA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, amepiga marufuku hospitali za umma na binafsi kuwatoza wananchi fedha kwa ajili ya chanjo ya corona...

## Sabaya augua ghafla mahabusu

UKURASA 2

**MICHEZO** **LIGI KUU BARA SEPT. 29** UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Sabaya adaiwa kuugua gerezani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imeahirisha kusikiliza kesi ya jinai namba 105, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34).

Hatua hiyo inatokana na baada ya mshtakiwa huyo kushindwa kufika mahakamani kutokana na tatizo la kiafya.

Mbali na Ole Sabaya washtakiwa wengine wawili katika shauri hilo la jinai lenye mashtaka matatu ni Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38).

Akizungumza mahakamani huko jana, Wakili Mkuu wa Serikali, Tumaini Kweka, alidai waliwasiliana na uongozi wa Jeshi la Magereza na uliwajulisha kuwa mshtakiwa wa kwanza (Ole Sabaya) ameshindwa kufika mahakamani kwa kuwa ni mgonjwa.

Wakili huyo alidai ni matakwa ya kisheria chini ya kifungu cha 196, kinachosimamia mwenendo wa makosa ya jinai Sura ya 20, kwamba usikilizwaji, uchukuaji na utoaji wa ushahidi lazima mshtakiwa awe mahakamani.

Hata hivyo, alidai kifungu cha 197 cha mashauri ya jinai kimeweka utaratibu wa kusikilizwa kwa shauri pasipo kuwapo kwa shahidi mahakamani.

Alidai, pia sheria inaelekeza kama mshtakiwa ametoa ridhaa kwa wakili wake pasipo yeye kuwapo mahakamani usikilizwaji wa shauri unaweza kuendelea.

Wakili wa Utetezi, Dancan Oola, alidai mahakamani huko kwamba hawajapewa ridhaa na mshtakiwa kuendelea kusikilizwa kwa shauri hilo, hivyo aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kuendelea kusikilizwa kwa shauri hilo.

Mkaguzi Msaidizi wa Magereza, Ramadhani Misanga, alidai mahakamani kwamba kwa kawaida mahabusu kila siku wanafunguliwa kwenda kupata kifungua kinywa asubuhi na washtakiwa au wafungwa wenye matatizo ya kiafya wanakwenda kituo cha afya kwa ajili ya kupata huduma za kiafya.

Alidai mahakamani huko kuwa baada ya Ole Sabaya kwenda kituo cha afya kupatiwa matibabu, alimjulisha kuwa amepewa dawa na anatakiwa kupumzika kwa muda wa siku moja, hivyo hataweza kwenda mahakamani kwa ajili kuendelea kusikiliza shauri linalowakabili.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amworo, aliahirisha kusikilizwa kwa shauri hilo hadi leo.

Juzi, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdalah Chavula, Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Arusha, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP), Gwakisa Minga, ambaye ni shahidi wa saba wa Jamhuri, alidai kitendo cha kupiga, kutesa, kuteka nyara, kupora Sh. 390,000 na kuvamia duka la Mohamed Saad, kilichodaiwa kufanywa na Ole Sabaya, ni kinyume cha sheria za nchi.

Shahidi huyo alidai kitendo hicho ni kinyume cha sheria kwa kuwa mshtakiwa huyo hakuwa na kibali chochote cha kupekua na kuwakamata wafanyabiashara hao.

# Waziri wa Marekani kuteta na CHADEMA

**Na Waandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Victoria Nuland na timu yake wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan wafanye mazungumzo na vyama vya upinzani nchini kikiwamo chama kikuu, CHADEMA.

Miongoni mwa ajenda za timu hiyo kutoka Marekani ni kutaka kufahamu chanzo cha kukamatwa kwa Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alibainisha hayo jana alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu kuwapo taarifa za timu hiyo iliyotoka Marekani, kuomba kukutana na vyama hivyo vya upinzani vya Tanzania.

"Ni kweli tuna ujumbe kutoka nchini Marekani ambao umekutana na Rais wetu na umeomba pia kukutana na vyama vya upinzani nchini kikiwamo CHADEMA hasa kutaka kujua suala hilo la kukamatwa kwa Mbowe.

"Rais amesema yeye hawezi kuwazuia kukutana na vyama hivyo isipokuwa ujumbe wa Serikali ya Tanzania bado ni kwamba nchi kwa sasa inashughulikia mambo makubwa ikiwamo suala la kukuza uchumi na kupambana na suala hili la janga la ugonjwa wa corona.

"Rais amesema ndio maana anataka mambo mengine yakae pembeni kwanza ili washughulikie mambo haya kwanza ambayo pia yanahitaji ushirikiano mkubwa wa kila mtu.

"Haya mambo mengine ya siasa inabidi yakae pembeni kwanza yasubiri na kama kukutana na atakutana navyo kwa sababu yakiingizwa mambo mengine wakati huu wa mapambano ya janga hili, itakuwa ni vigumu kushinda," Balozi Mulamula alifafanua.

Ujumbe huo umeomba kukutana na vyama hivyo vya upinzani katika kipindi ambacho tayari Mwenyekiti wa CHADEMA, Mbowe yuko mahabusu akikabiliwa na mashtaka ya ugaidi.

**■imeandaliwa na Elizabeth Zaya, Sechellah Nakamba na Haika Christopher (SJMC)**




Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Faustine Ndugulile (katikati), akikata utepe kuzindua huduma za CRDB Wakala kupitia Shirika la Posta, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wapili kushoto), Kaimu Postamasta Mkuu, Macrice Mbodo (wapili kulia), Mkurugenzi wa Mawasiliano Wizara hiyo, Clarence Ichwekeleza (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Biashara Benki ya CRDB, Toyi Ruvumbangu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto, Mbatia wamtembelea Mbowe Gereza Kuu Ukonga

**Na Romana Mallya**

KIONGOZI wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, na Mwenyekiti wa NCCR- Mageuzi, James Mbatia, wamemtembelea Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, gerezani Ukonga jijini Dar es Salaam alikowekwa mahabusu akikabiliwa na mashtaka ya ugaidi.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, ilibainisha kuwa viongozi hao wawili baada ya kuonana na Mbowe, pamoja na mambo mengine, walimwachia kitabu.

Nipashe ilimtafuta Zitto kuzungumzia suala hilo, akibainisha kuwa walifika gerezani huko majira ya saa tisa mchana na walimkuta akiwa vizuri na mwenye matumaini makubwa.

Julai 20, mwaka huu, Mbowe alikamatwa jijini Mwanza akiwa hotelini wakati akijiandaa kufanya kongamano la kudai Katiba mpya.

Baada ya kukamatwa, Mbowe alisafirisha kwenda Dar es Salaam, alikofanyiwa upekuzi nyumbani kwake, kisha kupelekwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi jijini kwa ajili ya mahojiano, lakini alidaiwa kutotoa ushirikiano.

Mbowe, mfanyabiashara na Mbunge wa zamani wa Hai mkoani Kilimanjaro, alishikiliwa kwenye Kituo cha Polisi Oysterbay hadi Julai 26, mwaka huu alipofikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kusomewa mashtaka ya ugaidi.

# Mbaroni kwa madai ya kumuua 'shamba boi', mwili wake kuufukia

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia watu wanne akiwamo mwanamke kwa tuhuma za mauaji ya mchunga mifugo, Shabani Mbalali (20), mkazi wa Chamanzi ambaye baada ya kumuua walimfukia na kuiba mbuzi watano.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema kijana huyo aliuawa na watu wasiofahamika Jumamosi iliyopita, eneo la Chamazi Vigoa akiwa machungani.

"Akiwa anachunga mbuzi eneo hilo, watu wasiofahamika walimuua na kuiba mbuzi watano na kisha mwili wake kuufukia kwenye shimo," alisema.

Muliro alisema katika ufuatiliaji walikamatwa watu wanne ambao ni Anold Kavishe (36) mkazi wa Maji Matitu, Justine Joseph (32) mkazi wa Kisewe, Selemani Hamisi (39) mkazi wa Chamazi na Joyce John (38) mkazi wa Maji Matitu.

Katika tukio lingine, Kamanda Muliro alisema wanawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kutishia kwa bastola wanazozimiliki.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Isack Willy (44), maarufu Wambura mkazi wa Sinza E, Rashid Mshana (36) na Mussa Mshana (39) wote wakazi wa Mwenge na Ibrahim Shaibu (52) mkazi wa Kinyerezi.

Alisema mtuhumiwa Willy akiwa baa iitwayo 99 Vibes maeneo ya Sinza, alitoa silaha aina ya Browning na kudaiwa kutishia watu akiwa amelewa.

"Mtuhumiwa Rashid alionekana kwenye 'video clip' iliyosambaa mtandao wa kijamii akitishia kwa silaha aina ya Browning. Tulifanya upelelezi na kumkamata na silaha yake ikiwa na risasi 10 ndani ya magazine. Silaha hiyo inamilikiwa na kaka yake Mussa," alisema. Alisema Mussa anatuhumiwa kwa kosa la uzembe kwa kumwachia silaha mdogo wake ambaye ni Rashid aliyejirekodi akitishia watu na kudaiwa kutuma mtandaoni.

"Agosti Mosi jioni maeneo ya Vijibweni Kigamboni mtuhumiwa Ibrahim alimtishia kumuua kwa silaha jirani yake aliyefahamika kwa jina la Chacha Mwita walipokuwa wakigombea mipaka ya kiwanja. Alikamatwa na bastola aina ya Luger ikiwa na risasi sita," alisema.

Kamanda alisema silaha hizo zinashikiliwa wakati utaratibu wa kisheria ukifuata ikiwa ni pamoja na kuwafutia umiliki wake.

"Unapewa silaha alafu unaanza kuitoa ovyo ovyo pasipo sababu, kupewa silaha unataka watu wajue una silaha pasipo sababu ya msingi, katika mazingira ambayo hayaruhusiwi ikibainika tunafuata taratibu kama hawa, hizi si silaha za maonyesho kwenye maeneo yenu," alisema.

Alisema wanaendelea kufuatilia kwa ukaribu na halitasita kuwanyang'anya wakiwamo walevi wataosababisha silaha zikaingia mikononi mwa wahalifu.

# Adaiwa kujinyonga baada ya kubainika na maradhi ya UTI

**Na Halima Ikunji,** TABORA

VERONICA Thadeo (23), mkazi wa Kijiji cha Katungulu, Kata ya Usisya wilayani Urambo mkoani Tabora, amedaiwa kujinyonga baada ya kupima na kukutwa na maambukizi maradhi ya njia ya mkojo (U.T.I).

Akizungumza na Nipashe jana, Diwani wa Usisya, Aziza Galula, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kudai, kuwa Veronica aliacha ujumbe wa kuwaaga wazazi wake na kuelekeza fedha zake za mauzo ya tumbaku zikilipwa, apewe mama yake.

Alisema tukio hilo lilitokea Julai 30, mwaka huu, katika kijiji hicho majira saa 10 jioni, baada ya kutoka zahanati ya kijiji hicho kupima afya yake.

Diwani huyo alisema kuwa kabla ya kutokea kwa tukio hilo, Veronica alikuwa akisumbuliwa na homa na kwamba baba yake, Tadeo Joseph, alimpeleka kwenye vipimo na waliporejea nyumbani aliamua kuchukua uamuzi huo.

"Alikuwa anaumwa japo hali yake haikuwa mbaya sana, baba yake akampa dozi ya mseto, lakini haikumsaidia na baada ya hapo waliamua kwenda zahanati ya hapa kijijini, alipopimwa alikutwa na U.T.I," alidai diwani huyo.

Alidai kuwa wamebaini binti huyo alijiua kwa kunywa vidonge vyote alivyopewa hospitali na baadaye kujinyonga nyuma ya nyumba yao, huku akiacha ujumbe.

"Baba na mama nimeamua kujiua, ninawatakia maisha mema. Pia kuna hela ya tumbaku ikitoka, basi hela zote achukue mama," ulisomeka hivyo ujumbe unaodaiwa kuandikwa na Veronica kabla ya umauti kumfika. Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ukondamoyo katika Kijiji cha Katungulu, Selemani Kapaya, ambaye ni jirani wa familia hiyo, alisema wamesikitishwa na tukio hilo na kutoa ushauri kwa wananchi wa kitongoji chake kuhakikisha halitokei tena.

Ilidaiwa kijijini huko kuwa, Veronica alikuwa akijishughulisha na ushonaji na kilimo cha tumbaku.

Baadhi ya majirani walisema binti huyo alikuwa mchapakazi na hakuwahi kuonyesha tabia mbaya hapo awali na alikuwa akishirikiana na jamii katika mambo mbalimbali na wamesikitishwa kwa kumpoteza.

Kamanda wa Polisi mkoani Tabora, Safia Jongo, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho na kuwataka wananchi kuacha kujichukulia kisheria mikononi.

Aliwataka wazazi kutekeleza kikamilifu wajibu wao wa msingi wa kukaa na familia zao na kusikiliza shida zinazowakabili vijana wao na kuzipatia majibu.

Alisema wanaendelea na uchunguzi wa kifo hicho na baada ya upelelezi, kukamilika watatoa taarifa ya kiini cha kifo hicho japo hakuna mtu yeyote anayeshikiliwa na jeshi hilo kutokana na tukio hilo.

NMB
Karibu yako

KUTOA HUDUMA BORA ZA KIBENKI
KWA WOTE NI JADI YETU

Tuzo ya Umahiri ya Euromoney
- Benki Bora Tanzania 2021, mara 9 mfululizo

Tuzo ya Global Banking & Finance - Benki Bora ya Wateja Binafsi na Biashara za Kati Tanzania 2021




Asante kwa Kuchagua NMB Bank!

#BoraKatikaUbora

216394102

www.nmbbank.co.tz

# SUA kutengeneza chanjo ya corona

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kwa kushirikiana Taasisi ya Taifa ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR) wameanza kufanya utafiti wa chanjo ya virusi vya corona, ili wazalishe chanjo hiyo nchini.

Akizungumza katika uzinduzi wa utoaji wa chanjo dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 katika chuo hicho jana, Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema lengo la kuzalisha chanjo hiyo ni kukidhi mahitaji ya chanjo nchini, ili isiagizwe kutoka nje ya nchi.

Alisema kwa sasa chanjo zote zilizoanza kutumika nchini zimeletwa kutoka nje ya nchi, lakini wao kama wasomi nchini kwa kutumia nafasi yao ya sehemu ya vyuo vikuu, wameona kuna haja kuanza kufanya utafiti wa pamoja, ili kukidhi mahitaji ya chanjo za ugonjwa huo, ambazo zitazalishwa nchini.

"Sisi kama sehemu ya taasisi za elimu ya juu nchini, tumeona tushirikiane na vyuo vingine vikuu kama Muhimbili na Taasisi ya NIMR tuanze sasa kuzalisha chanjo ya virusi vya corona, ili kuisaidia kupunguza makali na madhara ya virusi hivyo kwa taifa," alisema.

Akizungumzia kuhusu utoaji wa chanjo hiyo kwa jamii nzima, alisema baada ya chanjo hizo kupatikana katika Mkoa wa Morogoro, waliwasilisha ombi la kuwa na kituo katika chuo hicho kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi wapatao 15,000, pamoja na wafanyakazi 2,000, ambao wengi wao umri wao ni mkubwa.

Alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Morogoro pamoja na Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa kwa kukubali kuanzisha kituo hicho na kuwapa chanjo 500, kwa ajili ya hatua za mwanzo za kuchanja makundi maalum yenye sifa.

Profesa Chibunda alisema pamoja na uhaba wa chanjo walizopata, wanaamini wataongezewa kadri siku zinavyoendelea na watakavyopokea na kuitaka jamii kupuuza na kuacha kupotoshwa na baadhi ya watu katika mitandao kuwa chanjo hiyo ina madhara.

"Maprofesa hao wanachanjwa hapa ndio wamekuwa wakisafiri katika nchi nyingi duniani, sasa kama hii chanjo ingekuwa na madhara yoyote, wao ndio wangekuwa wa kwanza kutochanja, hebu tuachane na watu wanaopotosha kuhusu chanjo hii," alisema.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo na Kiongozi wa Madaktari wa Hospitali ya SUA, Dk. Omary Kasuwi, alisema anashukuru kupatikana kwa chanjo hiyo ya UVIKO-19, kwa kuwa itasaidia kupunguza kero za wagonjwa waliokuwa wakifika kupata matibabu katika hospitali hiyo.

Dk. Kasuwi alisema hospitali hiyo inayohudumia wanafunzi wa SUA, wafanyakazi na watu kutoka nje imeshapokea takribani wagonjwa 2,000, tangu kuibuka kwa ugonjwa huo wa corona na kuwapatia matibabu mbalimbali.

# Kiongozi CCM mbaroni tuhuma za kuuza ardhi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Picha ya Ndege, Kibaha Mjini, Godfrey Mwaipopo, ametiwa mbaroni kwa tuhuma za kuhusika kuuza ardhi kinyume cha taratibu na kusababisha migogoro katika eneo la Lulanzi.

Kukamatwa kwa mwenyekiti huyo ni maagizo ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliyoyatoa jana akiwa katika kikao na baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Lulanzi wanaokabiliana na mgogoro wa ardhi kwa muda mrefu ambao kwa sasa wanasubiri uamuzi wa kesi iliyoko mahakamani.

Akiwa katika kikao hicho, Kunenge aliagiza Mwaipopo pamoja na wenzake tisa kuwekwa chini ya ulinzi kwa mahojiano na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuuza shamba moja kwa zaidi ya mtu mmoja, hali ambayo inaleta sintofahamu kwa wakazi wa eneo la Lulanzi.

Kunenge alisema kiama cha vishoka wa ardhi katika mkoa huo kimefika kwa kuwa hayuko tayari kuendelea kumvumilia mtu yeyote atakayehusika na kuuza maeneo ambayo yana hati miliki kwa watu tofauti na kusababisha migogoro ya ardhi kuendelea katika mkoa huo na shughuli nyingine za maendeleo kusimama.

Alisema ana majina ya watuhumiwa 10 ambao wanahusishwa na uuzaji wa maeneo kinyume cha sheria huku wengine wakiuza eneo ambalo lina mgogoro na limewekewa zuio la kimahakama, jambo ambalo linaleta hofu ya kuvunjika kwa amani.

"Nimekuja Pwani kufanya kazi, nitatenda haki, ninataka wakazi wa mkoa huu kuheshimu sheria, mtandao wa matapeli wa ardhi mkae sawa, kazi ndio imeanza, hakuna kumwonea mtu hapa, kila kitu kitafanywa kwa kufuata sheria," alionya.

Akizungumzia eneo ambalo kwa sasa limewekewa zuio na mahakama, alisema kitu cha kushangaza ni kwamba bado wapo watu wanaendelea kutumia nyaraka feki na kuuza eneo hilo lenye mgogoro kati ya wananchi na familia ya Said Salim ambalo hadi sasa hukumu haijatolewa.

Alisema hakufika katika eneo hilo kuingilia mahakama kwa kubainisha nani mwenye haki kati ya Said Salim na wananchi, bali amefika kushughulika na wanaokiuka maelekezo ya mahakama na wale ambao wamekuwa wanatuhumiwa kuuza ardhi bila kufuata sheria.

"Tunataka tutoe funzo kwa vishoka, matapeli wa ardhi, hatutamwonea mtu wala kuogopa, kama ni wa chama tawala wala serikali au kiongozi yeyote.

"Katika hii operesheni ondoa migogoro ya ardhi, haki itatendeka kwa mujibu wa sheria," alisema. Kunenge alisema mtu ambaye ameuza shamba au kiwanja kimoja kwa watu wawili au zaidi, ni wazi ana hatarisha usalama kwa kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi katika mkoa huo na hastahili kuachwa.

Alimtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Kibaha kuhakikisha waliotajwa wakituhumiwa kushiriki kuuza ardhi kwa maeneo ambayo yana umiliki halali, wanakamatwa na kuhojiwa na hatua za kisheria zichukuliwe kukomesha tabia hiyo.




Mkuu wa Kitengo cha Wajasiriamali cha Benki ya NBC, Mussa Mwinyidaho (katikati), Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Kati, Moses Minja (kushoto) na Meneja wa Huduma mpya ya NBC Jamii Akaunti, Mwinyiusi Hamza, wakizindua rasmi huduma hiyo, jijini Dar es Salaam jana, ambayo ni mahsusi kwa ajili ya Taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs), taasisi za misaada na taasisi za kidini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi za kifedha zapewa mtihani kuwafikia wananchi wasio na huduma

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeagiza taasisi za fedha kuwafikia na kuwarasimisha Watanzania asilimia 35 kuingia kwenye mfumo rasmi wa huduma za kifedha kwa sababu kwa sasa haijulikani wanatumia njia gani.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa huduma za Benki ya CRDB Wakala katika ofisi za Shirika la Posta Tanzania. zaidi ya vituo 200 vimefunguliwa na lengo ni vifikie 350.

Dk. Ndugulile alisema takwimu za sasa zinaonyesha asilimia 16.7 ya Watanzania wanapata huduma za kifedha kwenye taasisi za benki, asilimia 48.6 wanatumia mitandao ya simu, asilimia 6.7 wanajua wenyewe huduma hizo wanazipata wapi na asilimia 28 hawana huduma zozote za kifedha.

"Hawa ni watu wengi tunahitaji tuwafikie asilimia 28 na kuwajumlisha asilimia 6.7 ambao wote kwa pamoja tunapata jumla yao asilimia 35. Hawa wanatakiwa kufikiwa," alisema.

Waziri huyo alisema utaratibu ambao Shirika la Posta na Benki ya CRDB wameuzindua siku hiyo wanaamini watakwenda kuwafikia asilimia 35 ya Watanzania hao.

"Miaka mitano au sita nyuma kwa sababu na mimi ni mteja wenu CRDB ulikuwa unakwenda kwenye tawi kwanza unaanza kutafuta namba ya meneja au ya mkurugenzi. Lakini nina muda mrefu sijampigia mtu yeyote simu maana yake huduma za wateja mmeziboresha," alisema.

Pia aliipongeza benki hiyo kwa kupanua wigo wa kutumia mawakala na kuwaeleza kuwa baadhi ya maeneo wapo ambao hawajafikiwa na kutaka waliangalie suala hilo.

Alisema kwa miezi minane akiwa ndani ya wizara hiyo, wamefanya mabadiliko katika sekta ya mawasiliano, Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kubadilisha utendaji wa kazi wa taasisi ikiwamo Shirika la Posta.

"Utendaji wa Shirika la Posta kwa sasa mnaanza kwenda vizuri. Ninaona mwelekeo ninaoutaka Posta niliyoikuta si wa sasa. Niwaambie benki ya CRDB tumefanya mabadiliko makubwa Posta kuwabadilisha mtazamo, mwelekeo, utendaji. Tunataka kutoka Posta ya kusambaza barua kuwa na stempu na kuziuza," alisema.

Alisema wanataka Shirika la Posta liwe kitovu cha kufanya biashara mtandao Tanzania na huko ndiko wanakoelekea.

"Kikubwa ni huduma ya pamoja kupitia kituo cha huduma ya pamoja kilichofunguliwa ofisi za Posta Tanzania kinachojumuisha taasisi za serikali ambapo sasa mwananchi hasumbuki kwenda kwenye ofisi zao, wanakuja Posta wanazipata katika eneo moja," alisema.

Dk. Ndugulile alisema wanatarajia kupata fedha kiasi cha Sh. bilioni 300 katika kutekeleza mradi wa Tanzania ya kidigitali.

"Eneo mojawapo ambalo tunataka kulibadilishe ni kwenda na Posta ya kidigital, huko tunakokwenda barua isije kuchukuliwa hapa, ndiyo maana ya Posta kiganjani.

"Upo mradi mwingine unaofanywa ndani ya wizara yangu wa anuani za makazi tunataka kila mtaa wako uwe na jina na kila nyumba iwe na namba na kila eneo iwe na anuani ya makazi, ili barua na vifurushi vyako vikufikie ulipo, serikali imetupa fedha nyingi," alisema.

HABARI KITAIFA

# Bastola ya DC yakamatwa ikifanya uhalifu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu watano kwa tuhuma za kukamatwa na bastola moja ikiwa na risasi 11.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema watu hao walikamatwa juzi katika maeneo ya Forest jijini Mbeya.

Alisema baada ya uchunguzi polisi walibaini kuwa bastola hiyo yenye namba za usajili TZCAR 73390-053639 ni mali ya Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, John Palingo. "Pistol moja aina ya Browning na risasi zake 11, tulibaini kuwa ni mali ya Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, John Palingo," alisema Kamanda Matei.

Hata hivyo Kamanda Matei hakueleza mazingira yaliyosababisha bastola hiyo kukutwa ikiwa mikononi mwa wahalifu.

Kamanda Matei aliwataja watu waliokamatwa na bastola hiyo kuwa ni Isaka William (24), Farew Raphael (30), Malodi Joseph (24), Daniel Kamwela (24) na Shadrack Msemwa (35), wote wakazi wa Iyunga jijini Mbeya.

"Mbali na bastola hiyo, watuhumiwa hawa pia tuliwakamata wakiwa na mali mbalimbali kama vile mikufu mitatu ya fedha, runinga tatu, simu moja, redio, begi a pete vitu ambavyo vinadhaniwa kuwa ni vya wizi," alisema Kamanda Matei.

Kamanda Matei alisema uchunguzi wa Jeshi la Polisi umebaini kuwa baadhi ya mali hizo ni za Beatrice Chande, mkazi wa mtaa wa Forest jijini Mbeya ambazo zinadaiwa ziliporwa nyumbani kwake wakati mwenyewe akiwa safarini. Katika hatua nyingine Kamanda Matei alisema kuwa jeshi hilo limepata taarifa za kiintelijensia kuhusu watu wanaojiandaa kufanya maandano mkoani Mbeya, na aliwaonya wasijaribu.

Alisema mpaka sasa Jeshi la Polisi halijatoa kibali chochote cha kufanyika kwa maandamo mkoani Mbeya, endapo watu watajaribu kuandamana watakuwa wamefanya maandano yasiyo na kibali jambo ambalo ni kosa kisheria.

"Nimewasiliana na ma-OCD wangu katika wilaya zote hakuna mahali ambapo kuna kibalio cha maandamano kilichotolewa, hivyo nawasihi wananchi wajaribu kushiriki maandamano yoyote yasiyo na kibali kwa vile watakutana na mkono wa dola," alisema Kamanda Matei.

Kamanda Matei aliwaomba wananchi watoe taarifa za uhalifu na wahalifu ili hatua ziweze kuchukuliwa kwa kuhakikisha wananchi mkoani Mbeya wanaishi kwa amani na utulivu.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akizungumza wakati akifungua semina kwa wastaafu watarajiwa kuhusu elimu ya uwekezaji kwa maisha endelevu baada ya kustaafu, iliyoandaliwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba. **PICHA: JOHN BADI**

# Viongozi CHADEMA watiwa mbaroni

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

VIONGOZI sita wa Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) Mkoa wa Kagera, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa tuhuma za kukutana na kufanya kikao cha kushinikiza kuachiwa huru kwa Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revokatus Malimi, alibainisha kukamatwa kwa viongozi hao jana alipozungumza na vyombo vya habari mjini Bukoba.

Malimi alisema viongozi hao walikamatwa jana baada ya jeshi hilo kupokea taarifa za kuwapo na kikao hicho.

Kamanda huyo alisema jambo lolote linapofikishwa mahakamani haliruhusiwi kujadiliwa sehemu yoyote tofauti na mahakamani.

"Jambo la mahakamani haliruhusiwi kujadiliwa na wananchi, hata vyama vyovyote haviruhusiwi, ni uchochezi na uvunjifu wa amani," alisema Kamanda Malimi

Alisema vyama vya siasa vinavyojaribu kufanya majadiliano ya kesi, ambayo ipo mahakamani vinakwenda kinyume cha sheria.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa CHADEMA Manispaa ya Bukoba, Victor Sherejey, alisema viongozi hao walikamatwa wakiwa katika ofisi za chama hicho wakisajili kadi zao kupitia mfumo wa kidigitali.

"Ni kweli viongozi wetu wamekamatwa leo (jana), walikuja hapa ofisini kwa ajili ya kujisajili kupitia CHADEMA Digital," alisema.

Kiongozi huyo alisema anashangaa Jeshi la polisi kuendelea kuwafanyia alichokiita uonevu kwa kuwa walikuwa ofisini kwao na hawakuwa na kikao cha aina yoyote, lakini wakakamatwa na kuambiwa walikuwa wanafanya mipango ya kumtetea Mbowe.

Alisema vyama vya siasa sio uhalifu, lakini anashangaa kuona polisi wanataka kulifanya lionekane hivyo ilhali wao wapo kwa mujibu wa sheria.

"Sasa hata ofisi zetu tusifungue, yaani tusifanye shughuli zozote za chama tukiwa ofisini kwetu?" alihoji. Aliwataja viongozi waliokamatwa kuwa ni pamoja na Specioza Kamala ambaye ni Katibu wa BAWACHA mkoani Kagera, Doris Herman, Mwenyekiti wa BAWACHA Kata ya Kashai na Odeta Gasper ambaye ni Katibu wa BAWACHA Kata ya Rwamishenyi.

Wengine ni Paulina Dilenge, Mwenyekiti wa BAWACHA Wilaya ya Muleba Kaskazini na Maidin Ibarahimu, Mwenyekiti wa BAWACHA Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera.

# Polisi wafanya operesheni Kibiti

**Na Romana Mallya**

OPERESHENI ya siku tatu ya Jeshi la Polisi iliyofanywa katika Wilaya za Kibiti, Mkuranga na Rufiji mkoani Pwani ili kubaini shughuli zozote za kiuhalifu ikiwamo viashiria vya kigaidi, imejiridhisha maeneo hayo kwa sasa ni shwari.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, katika taarifa yake aliyoitoa jana, alisema Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Kamishna Msaidizi wa Polisi Kungu Malulu, aliongoza operesheni hiyo iliyofanyika kuanzia Jumamosi iliyopita na kumalizika Jumatatu.

Aliwataka wengine walioshiriki operesheni hiyo ni maofisa, wakaguzi na askari wenye vyeo mbalimbali kutoka Dar es Salaam, Pwani na Rufiji.

"Jeshi la Polisi linaendelea kuwashukuru wananchi kwa ushirikiano wanaoendelea kutoa kwetu na kuwezesha kupata mafanikio katika kubaini, kuzuia na kupambana na uhalifu na wahalifu," alisema.

Misime alisema wanatoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano na pale watakapoona viashiria vyovyote vya kihalifu katika maeneo yao, watoe taarifa ili hatua stahiki zichukuliwe kwa wakati na kuepusha madhara.

"Jeshi la Polisi linaendelea kusisitiza umuhimu wa kila Mtanzania kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi na anayekwenda kinyume, tutamchukulia kuwa lengo lake ni kuvuruga amani na utulivu na hatutasita kumchukulia hatua stahiki kwa mujibu wa sheria," alionya.

Alisema jeshi hilo liliamua kufanya operesheni hiyo maalum ya kukagua maeneo yaliyokuwa maficho ya wahalifu wenye kujihusisha na matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha na matukio yenye mrengo wa kigaidi.

"Kama mnavyokumbuka eneo hilo la Rufiji kuanzia mwaka 2014 hadi 2017 lilikuwa na matukio ya mauaji, unyang'anyi wa kutumia silaha na vitendo vyenye mrengo wa kigaidi.

"Kazi kubwa ilifanywa na Jeshi la Polisi katika kipindi hicho kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama na wananchi na kufanikisha kuwapata wahalifu na silaha nyingi zikiwamo za kivita," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya operesheni hiyo ya miaka hiyo, Jeshi la Polisi liliona umuhimu wa kufanya nyingine kukagua maeneo yaliyokuwa yanatumiwa na wahalifu kwa kipindi hicho yakiwamo ya Wilaya ya Kibiti kama Rungungu na Nyambunda.

Alisema maeneo mengine yaliyochunguzwa ni ya Mkuranga katika eneo la Bupu na Mamndimkondo na Rufiji eneo la Nyamitumba Ngomboroni na Kifuru.

Pia alisema operesheni hiyo imefanyika katika mapori yanayopatikana maeneo hayo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu kuhusu huduma za kifedha ipewe msukumo

**WAZIRI** wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, jana alizindua huduma za kifedha za benki ya CRDB Wakala kupitia ofisi za Shirika la Posta ikiwa ni juhudi za benki hiyo kujipanua zaidi na kuongeza wigo wa huduma zake kwa wateja.

Shirika hilo kongwe la mawasiliano linakusudia kuwa na huduma za uwakala wa benki hiyo katika vituo 350 huku hadi sasa likiwa limeshaanzisha zaidi ya vituo 200.

Jambo kubwa lililojitokeza katika hafla hiyo ni kwamba hivi sasa takribani asilimia 35 ya Watanzania hawako kwenye mfumo rasmi wa huduma za kifedha kutokana na kwamba hawajui wanatumia njia gani.

Kwa mujibu wa Waziri Ndugulile, takwimu za sasa zinaonyesha asilimia 16.7 ya Watanzania wanapata huduma za kifedha kupitia benki, asilimia 48.6 mitandao ya simu, asilimia 6.7 wanajua wenyewe huduma hizo wanazipata wapi na asilimia 28 hawana huduma zozote za kifedha.

Idadi hiyo ya watu wasio kwenye mfumo wa huduma za kifedha ni wengi hasa katika zama za sasa za maendeleo ya sayansi na teknolojia hivyo wanatakiwa kufikiwa ili kunufaika na huduma hizo pamoja na usalama wao na fedha zao pia.

Hali hiyo inaonyesha wazi kuwa taasisi za kifedha zikiwamo benki na zile ndogo za kifedha, zina kibarua kizito cha kuhakikisha wananchi hao, wengi wakiwa wale waishio vijijini wanafikiwa ipasavyo.

Inawezekana kwamba watu hao, wengi wao wakiwa wakulima na wafugaji, wanahifadhi fedha zao kwa njia za kizamani ambazo zimepitwa na wakati kama vile kuweka kwenye michago ya vitanda vyao, kwenye vibuyu na kufukia ardhini.

Mfumo huo wa utunzaji fedha ambao unaweza kusababisha majanga kama vile kuvamiwa na majambazi na kuporwa, kuliwa na wanyama kama panga na kupata hasara kutokana na kuungua unapaswa kupigwa vita na kutokomezwa.

Njia kubwa na muhimu inayoweza kumaliza azma hiyo na watu kuingia katika mfumo wa kisasa kwenye ulimwengu wa kidigitali ni kutoa elimu juu ya utunzaji sahihi wa fedha ikiwamo kutunza kupitia benki na mtandao wa simu. Ni imani kwamba elimu hiyo ikifikishwa itabadilisha hata mawazo na fikra za watu ambao kwa namna fulani wanaamini kwamba wakiweka fedha zao benki wanaweza kuibiwa.


Katika miaka ya karibuni, kwa mfano, kumekuwa na jitihada za makusudi za taasisi za fedha kuwashirikisha wananchi katika mpango jumuishi wa fedha kwa lengo la kuwaelimisha wananchi kutumia vikundi au watu binafsi kuweka akiba katika benki.

Mpango huo, kutokana na takwimu zilizotolewa na Waziri kuhusu watu wasiofikiwa na huduma za kifedha, bado unahitajika zaidi katika kipindi cha sasa ili Watanzania waliosalia wanufaike na huduma hizo.

Lakini pia njia nyingine ni ya benki kutumia mawakala, njia ambayo imeenea sehemu nyingi maeneo ya mijini ambayo mteja halazimiki kufuata tawi la benki ili kufanya muamala wa kifedha. Njia hiyo ya wakala pia inapunguza gharama za mteja kutumia mrefu kuifuata huduma.

Ni wajibu sasa wa serikali kuwahimiza wadau wa sekta ya fedha na mitandao ya mawasiliano kuhakikisha elimu hiyo inatolewa ikiwamo uwekezaji wa huduma za kifedha maeneo ya vijijini ili Watanzania wote wanufaike.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tusikabidhi kadi za pikipiki zetu kwa waendeshaji wenyewe

Na Halfani Chusi

**WIZI** wa pikipiki na magari umekuwa kilio kikubwa kwa wamiliki wa vyombo hivyo, kila kukicha na lazima umsikie mtu analalamika kaibiwa ama gari au pikipiki, hali ambayo imekuwa endelevu kila siku.

Kuibwa huko kuna namna nyingi ambazo watu wamekuwa wakikumbwa navyo. Kuna wakati mwendesha bodaboda anaviziwa kwa mapanga, anadhuriwa na kuporwa chombo.

Pia kuna namna ya mwizi ya kumlaghai mwenye chombo na baadaye kuondoka nacho jumla. Pia, huwa kuna wizi ambao mtu anamwamini dereva wa chombo.

Hapo inatokea mmiliki anamkabidhi dereva kadi ya chombo ma akiamwamini au lolote lile la kumlaghai na inaishia, mwendesha pikipiki hizo za biashara anatokomea nayo kwenda kuiuza.

Hapo kuna funzo. Kwa maana gani? Ni kwamba vituo vingi vya polisi kuna kesi za namna hiyo na niliwahi kuhudhuria shauri katika kituo kimojawapo cha polisi, kwa masikio yangu nikamsikia mtu anayelalamika pikipiki yake kuuzwa na mwajiriwa, dereva wa bodaboda.

"Nilimpa dereva wangu pikipiki afanye kazi, siku chache baadaye akanifuata akaniomba kadi ya pikipiki kwa madai anaenda kujiunga Uba (mtandao wa usafiri wa kukodi).

"Mimi sikujua kuwa kadi hiyo ya pikipiki yenyewe nikamwamini nikampa kadi, toka hapo sijawahi kumwona tena kumbe pikipiki alienda kuuza baada ya kufanikiwa kunilaghai na kumpa kadi, alisimulia.

Hapo nikajifunza kwamba kuna umuhimu mkubwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuweka utaratibu wa kuweka namba ya simu ya mmiliki wa chombo cha moto kwenye kadi, hali itayosaidia kumthibitishia kama muuzaji wa chombo kama ni mali yake halali au la.

Nalisema hili kwa sababu kama mnunuzi wa pikipiki au gari ataiona namba ya simu kwenye kadi anaweza kupiga simu na kumpata mhusika moja kwa moja hata kama mali imeibiwa pamoja na kadi.

Pia inawezekana kuwa rahisi kwa mnunuzi kujiridhisha kupitia namba hiyo ya simu na kama chombo muuzaji ama katumwa au kaiba.

Huwa kuna uwezekano wa mwizi kulazimisha kila kitu, katika kumridhisha mnunuzi wa mali, lakini namba ya simu inakuwa ngumu.

Mtu anaweza kufikia namna unampa dereva wako wa pikipiki pamoja na kadi labda ama kwa kumwamini au kulaghaiwa na ghafla simu yako inaita unapokea halafu mtu anasema "tunataka kununua pikipiki yako."

Hapo kunaibuliwa dhana kwamba wanaona haja ya kupiga simu kwako, kwa kuwa wanawasiliana kujua uhalali wa umiliki wa chombo.

Ni wazi mmiliki halali anajua kama kuna mpango wa kuuza ana atakataa nia hiyo na wakati huohuo, unajua kinachoendelea juu ya pikipiki na unaweza kuzuia biashara kufanyika pengine ikawa ndio msaada wa kuto potea kwa mali yako.

Kwa hiyo, katika kulitazama hilo kwa kina kuna kila sababu ya TRA kuongeza kipengele cha namba ya simu ya mmiliki wa chombo kwa usalama wa chombo cha moto cha mmiliki, ili mtu yeyote atakapotaka kununua pikipiki au gari lililotumika.

Kama anayemuuzia sio mhusika, atatakiwa kupiga namba ya simu iliyopo kwenye kadi, ili kuongea na mhusika halali kwa lengo la uthibitisho.

Sambamaba na kuwaomba TRA kuongeza kipengele cha namba ya mmiliki wa chombo, kila mmiliki anatakiwa kutambua kadi ya gari au pikipiki, haipaswi kupewa mtu ambaye sio mmiliki wa chombo hicho.

Vinginevyo ni pale kunakuwapo dharura au sababu maaluma inayotambulika kisheria, kama kadi inahitajika sehemu kama polisi kwa uthibitisho wa gari au pikipiki.

Pia, upande wa pili ni kosa la kumkabidhi mtu chombo cha moto na yake ni sawa na kumpatia akualize. Tujue, kadi ni sawa na namba ya siri iwe kwenye laini ya simu au kadi ya benki, kuachia ni kumruhusu mtu kukudhuru au kuiiba.

Mtu akizijua hizo namba, anaweza kukuibia pesa zako na kuna haja ya kuwa makini katik hali ambayo utekelezaji wake unaweza kupunguza wizi wa namna hiyo. Ni vyema kuwa na tahadhari kubwa.

**■Mwandishi anapatikana kwa namba ya simu: 0787879707.**

HABARI KITAIFA

# Mbunge aishukuru serikali Igunga kupewa mabilioni

**Na Mwandishi Wetu, IGUNGA**

MBUNGE wa Manonga, Seif Gulamali (CCM), ameishukuru serikali kwa kuipatia Sh. bilioni sita Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, ili kutatua kero za maji.

Gulamali alitoa pongezi hizo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali kutatua kero za maji jimboni kwake na wilayani Igunga kwa ujumla.

Alisema ukarabati wa visima vya kienyeji kwa kuviwekea pampu mpya na kukarabati visima ambavyo pampu zake zimekufa kwa baadhi ya vijiji, kikiwamo cha Buhekela.

Alisema kazi hiyo ilianza mwishoni mwa wiki iliyopita na inaendelea kwa visima vyote vya kienyeji kwenye jimbo zima la Manonga.

Alisema mkakati huo pia unajumuisha kuangalia njia bora ya kuchimba visima au kupeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye maeneo yote ambayo hakuna visima.

"Tunaishukuru serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa fedha walizotupatia Sh. bilioni sita kwa ajili ya kutatua shida ya maji wilayani kwetu Igunga.

"Tunasema asante sana kwa niaba ya wana Manonga," Gulamali alishukuru.

Mara tu ya kumalizika kwa Bunge la Bajeti Juni 30, mwaka huu, mbunge huyo alifanya ziara jimbo zima, akivifikia vijiji vyote 63 vya jimbo.



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule akipata chanjo ya Uviko 19, katika ukumbi wa Gedeko, mjini Geita jana. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# RC aonya watakaobainika kuuza chanjo ya corona

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

MKUU wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, amepiga marufuku hospitali za umma na binafsi kuwatoza wananchi fedha kwa ajili ya chanjo ya corona.

Akizungumza na wananchi kwenye uzinduzi wa chanjo hiyo uliofanyika jana kwenye ukumbi wa GEDECO mjini hapa, Senyamule alisema hospitali yoyote itakayogundulika ikiuza chanjo hiyo, itachukuliwa hatua kali za kisheria.

Senyamule alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kila mwananchi anapata chanjo ya corona ili kazi hiyo ifanyike kwa uadilifu na kwa haki na kwa walengwa wote kwa sasa.

Alisema kwa awamu ya kwanza mkoa wa Geita unatarajia kuchanja watu 50,000 katika vituo 18 na kuwataka wananchi kujitokeza kwa wingi ili kupata chanjo hiyo.

Pia alisema Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea kuwashauri wananchi kuendelea kujikinga na corona kwa kunawa mikono, kwa kuvaa barakoa, kwa kukaa umbali wa mita moja au zaidi na kuepuka msongamano pamoja na kufanya mazoezi.

Alisema viongozi wa dini na wananchi kuendelea kuombea ugonjwa huu wa Uviko-19 uweze kuondoka hapa nchini ili watu waendelee kukuza uchumi wa Taifa.

# Rwanda kutumia Kiswahili kama lugha taifa

**Elizabeth Zaya, Sechellah Nakamba, Haika Christopher (SJMC)**

SERIKALI ya Rwanda inatarajia kuanza kutumia lugha ya Kiswahili kama miongoni mwa lugha ya taifa ya nchi hiyo.

Pia, imesema iko tayari kuingiza lugha hiyo ya Kiswahili kwenye mitaala yao ili ianze kufundishwa shuleni.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuelezea ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoifanya nchini Rwanda.

Balozi Mulamula alisema ili kufanikisha mpango wao wa kutumia lugha ya Kiswahili, nchi hiyo imeomba kupelekewa timu ya wataalamu wa lugha hiyo ambao watasaidia kutengeneza mitaala ya kufundishia shuleni.

"Mpango wetu kama Tanzania ni kuuza lugha ya Kiswahili katika mataifa mbalimbali na tunaona hili limeanza kufanikiwa, tumefanya hivyo katika nchi mbalimbali na Rwanda nako tumepata fursa hiyo," alisema Balozi Mulamula.

"Tunataka kupitia lugha hii ya Kiswahili itumike kama fursa ya ajira. Kikubwa tunachosisitiza hapa ni watu kuchangamkia fursa hii, wakichelewa watajikuta watu wengine wanaichangamkia. Ndiyo maana tunawaomba mtusaidie kuelimisha kuhusu hili."

Balozi Mulamula alisema baada ya makubaliano hayo, Rais Samia aliagiza Wizara hiyo ya Mambo ya Nje, Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), kukutana na kupanga namna ya kulifanyia kazi suala hilo la kupeleka wataalam wa lugha ya Kiswahili nchini humo.

"Kwa hiyo tumejipanga kukutana sisi wote tulioagizwa kushughulikia suala hili kujadili kwa haraka sana namna tutakavyojipanga kuchangamkia fursa hii ambayo tumeipata ambayo kiukweli tumekuwa tukipambana kuipata katika nchi mbalimbali," alisema Balozi Mulamula.


The Guardian Limited

VACANCY

Freelancer Sales Executive

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

Responsibilities

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

Qualifications

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

NOTE: This is a commission Based Position

Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.

216387602

# Mawakala kuisaidia TCB kuinua huduma jumuishi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) inayomilikiwa na serikali, imepanga kupanua wigo wa upatikanaji wa hudumu zake kwa kuongeza idadi ya mawakala inaowatumia hadi kufikia zaidi ya 10,000, ndani ya miaka mitatu ijayo.

Mpango huo ni sehemu ya mkakati wa TCB kuimarisha huduma jumuishi za kifedha nchini na kuwahudumia zaidi Watanzania wa kawaida huku ikiwajumuisha katika mfumo rasmi wa fedha.

Hiyo ni kwa mujibu wa maofisa waandamizi wa benki hiyo ambao wamebainisha kwa sasa idadi ya mawakala wa TCB nchi nzima ni zaidi ya 3,500.

Mpango huo wa kuongeza idadi ya mawakala uliwekwa wazi mwanzoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kutia saini makubaliano na kuzindua upya ushirikiano kati ya TCB na Benki ya Standard Chartered Bank (SCB) Tanzania.

"Huduma jumuishi za kifedha ni suala nyeti la kimkakati kwetu kiutendaji na kupitia mawakala wetu zaidi ya 3,500, tumefanikiwa kuzisogeza huduma za kibenki karibu na makazi ya watu na biashara zao.

"Ndani ya miaka mitatu ijayo, tunapanga kuongeza idadi ya mawakala hadi kufikia zaidi ya 10,000," Mkurugenzi wa Teknolojia na Utendaji wa TCB, Jema Msuya, alifafanua baada ya kutiwa saini kwa makubaliano yao mapya na SCB Jumatatu iliyopita.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi, alisema makubaliano hayo pia yataimarisha ushirikiano kati ya benki hizo kufanya kazi pamoja kuwahudumia wateja wao.

Alisema chini ya utaratibu mpya wa kushirikiana, wateja wa SCB sasa watakuwa na wigo mpana wa kuhudumiwa na zaidi ya matawi 90 ya TCB pamoja na mawakala wake.

Awali, ushirikiano baina ya benki hizo uliihusisha mikoa ya Mbeya, Tabora, Kagera na Dodoma.

"Benki yetu ina matawi kamili 48, madogo 36 na zaidi ya mawakala 3,500 nchi nzima. Ushirikiano na SCB pia, utawawezesha baadhi ya wateja wetu kufanya miamala ya biashara kupitia benki hiyo, hivyo kuongeza shughuli za kibiashara za benki zetu,"alibainisha.

Kimsingi, ushirikiano huo wa kimkakati unawawezesha wateja wa SCB kuhudumiwa kupitia mifumo ya TCB kwenye maeneo ambapo huduma zake hazipatikani.

Moshingi alisema kwa kuwa kuyaendesha matawi ni ghali, ushirikiano wao unaiwezesha SCB kutatua kero za kiutendaji kwa ufanisi mkubwa.

Alisema utaratibu huu pia unainufaisha TCB kwenye upande wa nyanja za biashara za kimataifa ambako SCB iko vizuri na ina wigo mpana katika masoko mengi.

"Leo (Jumatatu) tunasaini upya makubaliano yetu na kuupa nguvu ushirikiano wetu, ambao ulianza miaka sita iliyopita. Ni ushirikiano muhimu kwa sababu Benki ya Standard Chartered ina matawi machache nchini na si ushirikiano wa bure," Moshingi alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija (wanne kulia), na Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard (watatu kulia), wakimkabidhi Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Wasioona Tanzania (TAB), Omar Itambu, sehemu ya fimbo 500 za kuongozea wasioona zenye thamani ya Sh. milioni 14, uliotolewa na Benki ya NMB, jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia (kulia) ni maofisa waandamizi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aagiza uchunguzi mradi wa TASAF

**Na James Mwanamyoto,**
MPANDA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi ameiagia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Katavi kufanya uchunguzi wa ujenzi wa mradi wa jengo la karakana ya wenye mahitaji maalum mkoani hapa.

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ulitoa fedha kwa ajili ya kuwezesha ujenzi huo ambao haujakamilika mpaka sasa.

Akizungumza jana na viongozi wa Chama cha Wenye Ulemavu Mkoa wa Katavi ambao ndio waasisi wa mradi huo, Ndejembi alisema TASAF ilitoa fedha kwa ajili ya kuwawezesha wenye ulemavu mkoani Katavi kujenga karakana hiyo ili kufanya shughuli zao kwa lengo la kuwawezesha kiuchumi.

Ndejembi alisema watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii na licha ya kuwa na ulemavu wameonyesha dhamira ya kujishughulisha na kutoa mchango kwa maendeleo ya taifa, hivyo wanapaswa kuungwa mkono na serikali na jamii kwa ujumla.

Aliongeza kuwa chama hicho kiliibua wazo la kuanzisha mradi huo ili wajishughulishe na ushonaji na kuwa na ofisi ya kikundi ambayo itaratibu ushiriki katika uzalishaji kwa manufaa ya taifa, hivyo atakaa na uongozi wa TASAF ili kuangalia namna ya kuwezesha ukamilishaji wa ujenzi huo baada ya uchunguzi wa TAKUKURU kukamilika.

Naibu Waziri alisisitiza umuhimu wa TAKUKURU kukamilisha uchunguzi kabla ya kuendelea na ujenzi wa mradi huo, lengo likiwa ni kujiridhisha na matumizi ya fedha zilizotolewa awali pamoja na kulinda hadhi ya Mwenge wa Uhuru ambao kiongozi wake aliweka jiwe la msingi Septemba 20, mwaka huu.

Pia alizungumzia hoja ya mgogoro wa kiwanja uliowasilishwa na viongozi wa chama cha wenye ulemavu waliodai kiwanja chao kuvamiwa na kumwelekeza Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Jamila Yusuph, kujiridhisha na mmiliki halali ili fedha zikipatikana ujenzi uanze mara moja badala ya kuanza kutatua mgogoro.

Naye Katibu wa Chama cha Wenye Ulemavu Mkoa wa Katavi, Godfrey Sadala, alisema lengo la kujenga karakana hiyo ni kutoa fursa kwa walemavu wengine mkoani humo ili wapate eneo la kujifunza na kuondokana na dhana potofu kuwa mtu akiwa mlemavu hawezi kufanya shughuli yoyote ya maendeleo.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Joshua Sankala, alisema mradi huo uliibuliwa kipindi cha pili cha TASAF ili kusaidia watu wenye ulemavu kufanya shughuli zao zitakazowakwamua kiuchumi.

Katika hatua nyingine, Ndejembi aliwasisitiza walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Kijiji cha Kawanzige, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda kutumia ruzuku wanayoipata kuboresha maisha yao.

Alisema mpango huo ulianzishwa na serikali kwa lengo kuboresha maisha ya kaya maskini ndiyo maana katika kijiji cha Kawanzige pekee Sh. milioni 118 zimetolewa kwa walengwa badala ya kupelekwa kwenye shughuli nyingine za maendeleo.

# Wazee wapewa neno chanjo ya corona

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZEE wameshauriwa kutumia fursa ya chanjo dhidi ya ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona (UVIKO- 19) ili kuimarisha kinga ya miili yao kipindi hiki ambacho serikali imewapa kipaumbele.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alitoa wito huo wakati akizungumza na wajumbe wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) waliomtembelea ofisini kwake, jijini Dodoma.

Dk. Jingu alisisitiza kuwa wakati huu ambapo dunia inapambana na maambukizi ya UVIKO- 19, makundi mbalimbali yanatakiwa kushiriki kikamilifu kuhakikisha janga hilo linatokomezwa.

"Kupitia mabaraza ya wazee, wawahamasishe wanachama wao kujitokeza kwa hiari kupata chanjo hiyo," alisema na kuongeza:

"Wazee ni kundi ambalo lipo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya UVIKO-19, hivyo jamii ihamasishe wazee wote kwenda katika vituo vya kutolea chanjo na kupata huduma hiyo."

Alisema wazee ni tunu ya taifa, hivyo jamii ina wajibu wa kuwalinda na majanga mbalimbali ikiwamo kuimarisha usalama wa afya zao.

"Uzee na kuzeeka unaambatana na changamoto ya kupungua kwa kinga ya mwili, hivyo serikali inatoa wito kwa wazee wote nchini kujitokeza kutumia fursa ya chanjo ya UVIKO- 19," alisema.

Aidha, Dk. Jingu aliwataka maofisa ustawi na maendeleo ya jamii wote kuhakikisha wazee wanaokwenda kupata chanjo kwenye vituo katika maeneo yao wanapata huduma zote wanazostahili bila usumbufu wa aina yoyote.

# Benki ya NBC yawafunda wastaafu watarajiwa

**Na Mwandishi Wetu**

WATUMISHI wanaotarajiwa kustaafu katika taasisi za serikali na mashirika binafsi, wametakiwa kuweka mikakati thabiti ya matumizi bora ya fedha sambamba na kupata elimu sahihi kuhusu huduma za kifedha na uwekezaji wa miradi sahihi ili wafaidike na mafao yao baada ya kukoma utumishi.

Viongozi waandamizi wa NBC katika mikoa ya Morogoro, Mtwara na Zanzibar walisema hayo walipopata fursa ya kuzungumza na wastaafu hao watarajiwa kwenye semina ya siku mbili iliyoandaliwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na kudhaminiwa na wadau mbalimbali ikiwamo benki hiyo.

Akizungumza kwenye moja ya semina hizo mkoani Morogoro, Meneja Mikopo wa NBC, Mtenya Cheya, aliwataka watumishi hao kuheshimu na kutunza fedha katika taasisi zinazoaminika sambamba na kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato kwa kufuata ushauri madhubuti kutoka kwa wataalamu.

"NBC tumejipanga kuwasaidia wastaafu watarajiwa na wale waliokwishastaafu ndiyo maana pamoja na kushiriki kwenye semina za mafunzo kama hizi, pia tumekuwa na mikakati na huduma bora kwa wastaafu ikiwamo kutoa mikopo inayozingatia mahitaji yao," alisema.

Katika semina kama hiyo iliyofanyika mkoani Mtwara, Meneja wa NBC Tawi la Mtwara, Emmanuel Mseti, aliwataka wastaafu hao watarajiwa kuhakikisha wanawashirikisha wataalamu wa fedha pindi wanapofikiria kuhusu mawazo ya biashara, uwekezaji na matumizi sahihi ya mikopo ili kujihakikishia ufanisi wa matumizi ya mafao yao.

"Ndio maana Benki ya NBC tumekuwa na utaratibu mzuri wa kuwapatia mafunzo wateja wetu kupitia mipango mbalimbali ukiwamo mpango wa klabu za biashara na utoaji wa mafunzo ya ujasiriamali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Lengo ni kuwajengea uwezo kufanya biashara kabla hatujawakopesha," alisema.

Wito kama huo pia ulitolewa Zanzibar na Mkuu wa Bidhaa na Mauzo wa Benki hiyo, Abel Kaseko, aliyewasihi wastaafu hao watarajiwa kuhakikisha wanahifadhi pesa zao kwenye taasisi rasmi za kifedha ili kuepuka matapeli.

"Zaidi pia tuhakikishe tunaanza uwekezaji mapema ili kujijengea uzoefu utakaotusaidia kujiandaa na maisha ya baadaye. Ifahamike kwamba matumizi sahihi ya fedha hizi ndiyo yatakayosaidia wengi wetu kuondokana na utegemezi baada ya kustaafu," alisema.

Pamoja na kuishukuru benki hiyo kwa nasaha hizo muhimu, washiriki wa mafunzo hayo kutoka katika taasisi mbalimbali walielezea namna walivyonufaika na mafunzo hayo. Pia walikiri kwamba wengi wao wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kushindwa kujiwekea akiba, matumizi yasiyo sahihi ya mafao baada ya kustaafu na kushindwa kubuni mawazo mazuri ya uwekezaji wa fedha hizo.

"Niwashukuru sana watu wa PSSSF kwa kuhusisha wataalamu mbalimbali kwenye semina hizi zikiwamo benki kama NBC kwa kuwa wametufumbua macho kwenye mambo mengi. Kwa kweli kupitia elimu hiyo itatusaidia sana," alisema Ali Mselem Ali, mstaafu mtarajiwa kutoka Zanzibar.

Semina hiyo ilipambwa na uwepo wa viongozi waandamizi wa serikali katika mikoa hiyo wakiwamo Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti.

## Watakiwa kuwapuuza wanaopotosha corona

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wametakiwa kuachana na mawazo potofu kuhusu chanjo ya corona kwamba zina madhara badala yake waendelee kujitokeza kwa wingi kuchanjwa kama ambavyo imekuwa ikielekezwa.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, alisema ni vyema Watanzania wakaachana na mawazo potofu na kuchukua hatua kama alivyofanya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Kama ambavyo ilitokea wakati wa utawala wa awamu ya tano tukakubali tulivyoelekezwa na serikali, ndivyo tunavyotakiwa kufanya kwa kufuata maelekezo ya serikali ya awamu ya sita," alisema Ngawaiya.

Alisema Watanzania hawapaswi kuendelea kuwa na msimamo wa serikali ya awamu iliyopita kuhusu corona, badala yake wafuate kile ambacho kinaelekezwa na serikali ilioko madarakani.

"Sisi watu tunaojishughulisha na utawala bora, tunaona ni sahihi Watanzania kuzingatia maelekezo ya serikali, kwani tunaamini kwamba haiwezi kukubali kuangamiza watu wake," alisema.

Alisema taasisi hiyo inatambua uhuru wa mtu kutoa maoni yake, lakini alisisitiza kuwa kwenye suala la chanjo, ni vyema maoni hayo yakawa sahihi kwa lengo la kusaidia Watanzania kuepuka ugonjwa huo.

"Rais alisema, chanjo hizo zimethibitishwa na Wizara ya Afya, hivyo wenye mawazo potofu wasaidiwe ili waachane nayo, kwani katika utawala bora, kiongozi wa nchi hawezi kuingiza wananchi wake kwenye matatizo," alisema.

Pia alisema hatua ya Rais kupokea chanjo na kuwa wa kwanza kuchanjwa, ilitosha kuwafanya Watanzania waamini na siyo kuendelea kupeana taarifa potofu kwenye mitandao.

"Yaani ni kwamba, imani waliokuwa nayo katika maelekezo ya serikali kwenye utawala wa awamu ya tano, ndiyo hiyo wanayopaswa kuwa nayo hata kwa serikali ya awamu ya sita," alisema.

Ngawaiya alisema dhana potofu ambazo zimekuwa zikipewa nafasi kubwa na baadhi ya watu kuwa chanjo za corona zimewahishwa au Watanzania wanatumika kufanyiwa majaribio, hazipaswi kupewa nafasi.

"Watanzania hawapaswi kuendelea kuwa na mashaka wakati Rais wao ameshaonyesha mfano, lakini imani waliokuwa nayo kuhusu corona, wakati wa awamu ya tano, hapaswi kuendelea kuikumbatia," alisema.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakidhibiti uvujaji wa maji katika bomba la inchi 10, eneo la Kimara, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kanisa lageukia uwekezaji elimu

**Ahmed Makongo,** BUNDA

KANISA la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Mara, limesema limejikita katika kuwekeza kwenye elimu, ili kuunga mkono juhudi za serikali katika sekta hiyo ambayo ni muhimu katika kuleta maendeleo ya wananchi.

Sambamba na hilo, kanisa hilo limewashauri wazazi na walezi kuwekeza kwenye mambo ya elimu kwa kuwasomesha watoto ikiwa ni pamoja na kuwalea katika maadili mema.

Wazazi pia wameshauriwa kuwafundisha watoto wao kuvichukia vitendo viovu vikiwamo vya uvunjifu wa amani, wizi na rushwa wakiwa na umri mdogo ili wanapofikia umri mkubwa wawe walimu wa kutoa elimu hiyo kwa jamii nzima kuvichukia na kutokujihusisha na vitendo hivyo.

Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mara, George Okoth, alibainisha hayo na kutoa ushauri wakati wa maombezi maalumu ya kuombea ujenzi wa mabweni mawili ya wasichana na wavulana katika shule ya Msingi Shalom iliyoko katika mji wa Bunda.

Askofu Okoth alisema kanisa hilo liko katika mstari wa mbele katika kuwekeza kwenye elimu kwa kuwa ni nyenzo pekee inayoondoa umaskini ndani ya jamii.

Kwa mujibu wa askofu huyo, kanisa hilo kwa kutambua umuhimu wa elimu, limekuwa likijenga shule katika maeneo mbalimbali na kwamba sasa limeamua kujenga mabweni hayo mawili katika shule hiyo, ili wanafunzi waishi shuleni hapo na kupata elimu pamoja na malezi bora, sambamba na kuwakinga na vishawishi vya kukatisha masomo pindi wawapo nje ya shule hiyo.

"Kanisa la Anglikana Tanzania linatambua umuhimu wa elimu ndiyo maana tumekuwa tukiwekeza kwenye elimu kwa kujenga shule pamoja na mabweni katika shule zetu. Hii ni hatua mojawapo ya kuunga mkono juhudi za serikali katika suala zima la elimu.

"Hivyo wazazi na walezi leteni watoto wenu katika shule zetu wapata elimu iliyo bora itakayowasaidia katika maisha yao ya baadaye na kuondokana na umaskini," alisema.

Alisema ni wajibu wa wazazi na walezi kulea watoto wao katika maadili mema ili waviache vitendo viovu vinavyomchukiza Mwenyezi Mungu.

"Kwa msingi huo ni jukumu la wazazi na walezi pia kuwalea watoto wao katika msingi wa kuwa na maadili mema ndani ya jamii inayowazunguka," alisisitiza.

Mkurugenzi wa Idara ya Elimu katika Dayosisi ya Mara, Arthur Mauya, alisema mabweni hayo yatakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 72 wa kike na wa kiume na ujenzi wake utakamilika baada ya miezi mitatu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mrefu Construction Co. Ltd, ambayo inajenga mabweni hayo, Kulwa Kahabi, alitumia fursa hiyo kwa kutoa wito kwa watu wenye kampuni za ujenzi kuwa waaminifu pindi wanapopata kazi za ujenzi ili kuaminiwa na kupewa kazi zaidi.

Wanafunzi wanaosoma katika shule hiyo walilishukuru kanisa kwa kuwajali na kuwapa malezi mema na elimu bora pamoja na kuwajengea mabweni hayo ili waishi shuleni hapo wakati wote wa masomo.

# Mbaroni tuhuma kukutwa na meno ya tembo kwenye banda la mbuzi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

JESHI la Polisi mkoani Katavi, linamshikilia Mathias Sikazwe (68), kwa tuhuma za kukutwa na meno mawili ya tembo akiwa ameyahifadhi kwenye banda la kufugia mbuzi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema tukio hilo lilitokea juzi katika Kijiji cha Igongwe Kata ya Stalike. Kuzaga alisema kwa kushirikiana na kikosi cha Hifadhi ya Taifa ya Katavi walipata taarifa kutoka kwa raia mwema na kuamua kufanya msako katika nyumba yake na kufanikiwa kumkamata.

"Meno hayo yana uzito wa kilogramu 2.5 ambayo thamani yake bado haijajulikana ila tunahesabu kwamba alimuua tembo mzima mwenye thamani ya Dola za Kimarekani 20,000," alisema Kuzaga.

Alisema Jeshi la Polisi bado linaendelea kumhoji mtu huyo ili kubaini washiriki wengine waliohusika na tukio hilo pamoja na kubaini silaha iliyotumika kumuua tembo huyo.

Kamanda Kuzaga alisema baada ya upelelezi kukamilika, taratibu zingine za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mtuhumiwa.

Katika hatua nyingine, Kuzaga alitoa wito kwa wananchi wanaojihusisha na shughuli haramu za ujangili kuacha mara moja na badala yake wafanye kazi za halali.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TCB, Sabasaba Moshingi (kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani, wakibadilishana mkataba, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini makubaliano ya kibenki ya kuhudumia wateja wa benki hizo, katika matawi yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamba aipiga jeki shule iliyoungua moto

**Na Thobias Mwanakatwe,** LUSHOTO

MBUNGE wa Bumbuli, January Makamba, ametimiza ahadi kwa kutoa msaada wa vitanda 20 vyenye thamani ya Sh. milioni nne katika Shule ya Sekondari Soni Day ambayo mabweni yake yaliteketea kwa moto.

Kutolewa kwa vitanda hivyo kunakamilisha ahadi yake aliyoitoa. Awali alitoa magodoro 100 na mabati 200 kwa shule hiyo ilipokumbwa na janga hilo.

"Wakati shule hii imekumbwa na kadhia ya janga la moto, nilitoa fedha zangu mfukoni na fedha kutoka kwa marafiki zake walinunua magodoro 100 na mabati 200. Ahadi iliyokuwa imebaki ni hii ya vitanda 20 sasa nimeikamilisha," alisema Makamba wakati akikabidhi vifaa hivyo kwa uongozi wa shule hiyo juzi.

Makamba alisema lengo la kusaidia katika shule hiyo ni kutaka kuunga mkono jitihada za kuinua kiwango cha elimu na ufaulu katika jimbo lake.

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Ally Lwena, alimshukru mbunge huyo kwa kusikia kilio hicho cha vitanda vya wanafunzi wa kike katika shule hiyo.

Lwena alisema hatua hiyo itasaidia kupata wanafunzi wengi watakaokaa hosteli, hivyo kuwaongezea muda mwingi wa kujisomea hatimaye kuongeze ufaulu wa shule na halmashauri kwa ujumla.

Mkuu huyo wa shule alisema kutokana na kukosekana kwa vitanda, wanafunzi walikuwa wakipigwa na baridi kali kutokana na kulala kwenye sakafu hali iliyosababisha magonjwa kama vile kukohoa, kubanwa na mbavu na hata vichomi.

Mwanafunzi wa kidato cha tatu, Mashoo Mrema, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema mabweni yao yalipoungua kwa moto mara mbili walikumbana na changamoto ya ukosefu wa vitanda hivyo kulazimika kulala chini kutokana na vitanda vilivyokuwapo kuungua wakati wa janga hilo.

Alisema kuwa msaada huo wa mbunge umekuja wakati muafaka wakati wao wakiwa na uhitaji wa vitanda hivyo.

Mrema alisema kuwa pia vitanda hivyo vitawasaidia kuwapa nguvu ya kujisomea na kuondokana na mawazo na magonjwa ya kukohoa waliyokuwa wanayapata kutokana na kulala chini.

# Kafulila ahimiza kodi bila shuruti

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amewataka wafanyabiashara mkoani hapa kulipa kodi bila shuruti kwa kuwa Tanzania ni moja ya nchi vinara barani Afrika na duniani kwa nidhamu ya matumizi ya kodi.

Aidha, amesema ripoti ya Jukwaa la Kiuchumi Duniani (WEF2019), inaitaja Tanzania kuwa nchi ya 29 duniani kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

Kafulila alisema hayo jana wakati wa kikao cha baraza la wadau wa kodi mkoani humo na kuongeza kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wanatakiwa kuhakikisha idadi ya walipa kodi inaongezeka.

"Tanzania ni chini ya 29 kati ya nchi 186 zilizofanyiwa utafiti kwa nidhamu ya matumizi mazuri ya fedha za umma hivyo ni vyema kulipa kodi maana inatumika vizuri kwa maendeleo ya watu wote," alisema.

"Mkoa una jumla ya walipa kodi 3,878 hii ni idadi ndogo sana ...ni muhimu kuongeza wigo wa walipa kodi ili kupunguza maumivu ya wale wanaolipa, lakini bado kuna ukwepaji kodi ...huu ni uvunjifu wa sheria," aliongeza.

Meneja wa TRA Mkoa wa Simiyu, Ernest Dundee, alisema jukwaa hilo ni fursa ya kuibua mambo ambayo yanaweza kushughulikiwa kisera.

Julius Mafuru, Meneja wa TRA Wilaya ya Maswa alisema madhumuni ya kuanzisha jukwaa la wadau wa mapato ni kuwezesha majadiliano kati yao na wadau ili kuimarisha usimamizi wa kodi.

**"Tanzania ni chini ya 29 kati ya nchi 186 zilizofanyiwa utafiti kwa nidhamu ya matumizi mazuri ya fedha za umma hivyo ni vyema kulipa kodi maana inatumika vizuri kwa maendeleo ya watu wote," alisema.**

ama
ALHAMISI AGOSTI 5, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

Ulinzi misitu ulivyowaletea maisha mapya wakazi wa Namtumbo na mazingira yao



Ukurasa 14

**Kitendawili cha agizo RC Makalla kusuasua wasafiri na wasafirishaji**

WIKI YA UNYONYESHAJI 2021

# Ushuhuda wa maziwa ya mama yalivyokuwa 'kila kitu' kwa mtoto

## •Hakuna magonjwa, darasani vinara

**Na Yasmine Protace**

UNYONYESHAJI watoto kwa kufuata taratibu wa wataalamu wa afya unamsaidia mtoto kukua vizuri, ikiwamo kuepuka magonjwa.

Kuna baadhi ya kinamama wazazi waliojifungua, wanaoshindwa kufuata kanuni za unyonyeshaji watachangia kuwaharibu watoto wao kiafya.

Ukweli uliopo ni kwamba, umuhimu wa unyonyeshaji unachangia watu kuwa na afya bora zaidi, hukua na kuwa na maendeleo mazuri wakilinganishwa na wale wanaolishwa maziwa yasiyo ya mama.

Namna walivyo watoto, wengi zaidi wangenyonyeshwa maziwa ya mama pekee, kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo ya maisha yao, bila ya kingine chochote, kiwe laini au kigumu.

Kanuni hiyo inawekwa bayana kwamba, afya ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, yangeweza kuokolewa kila mwaka.

Tafsiri pana ni kwamba, iwapo watoto wataendelea kunyonyeshwa hadi miaka miwili na zaidi, afya na maendeleo yao huwa bora zaidi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Cosmas Nshenye, hivi karibuni amezungumza kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, akiwa ba ufafanuzi, kwenye uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani



Mtoto akinyonya kwa mama yake. **PICHA: MTANDAO.**

**AMETAMKA:**

"Unyonyeshaji watoto maziwa ya mama ukifanyika ipasavyo kwa familia, jamii na taifa kwa ujumla, watoto wachanga watakuwa na hali nzuri ya lishe itakayoboresha ukuaji na maendeleo yao kimwili, kiakili na kasi ya itapunguza vifo na kasi ya magonjwa ya kuambukizwa."

Ni tamko alilotoa kwenye uzinduzi wa hafla hiyo kitaifa, uliofanyika wilayani Mbozi katika mkoa wa Songwe na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa lishe ya watoto wachanga na wadogo kitaifa.

Maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani Mwaka huu, 2021, yamebebwa na kaulimbiu inayosema "Kulinda Unyonyeshaji wa Maziwa ya Mama ni Jukumu Letu Sote."

Nshenye anasema, takwimu za ulishaji watoto nchini kwa mwaka 2018 zinaonyesha Tanzania imepiga hatua katika unyonyeshaji wa maziwa kwamba kuna wastani wa asilimia 92 ya watoto wanaendelea kunyonyeshwa maziwa ya mama pekee ndani ya miezi sita ya mwanzo wa maisha yao.

Pia, anataja takwimu za kitaifa kwamba, asilimia nyingine 87 ya watoto wanaanzishiwa vyakula vya nyongeza katika umri sahihi, yaani baada ya kuvuma miezi sita.

Kitaalamu, watoto wachanga wasionyoyeshwa maziwa ya mama, wapo hatarini zaidi kupata magonjwa au kupoteza maisha kwa maradhi, kwa sababu unyonyeshaji unawaongezea watoto kinga ya magonjwa kutoka kwa maziwa ya mama.

Mara zote, kunyonyesha watoto ni njia ya asili na inayohimizwa kulisha watoto wachanga, hata kama kuna vyakula mbadala.

Hivi karibuni, serikali imeitaka jamii kuwajibika katika ngazi zote kutetea, kulinda na kuendeleza utaratibu sahihi wa unyonyeshaji watoto maziwa ya mama, ili kuwajengea mazingira wezeshi kinamama waweze kunyonyesha watoto maziwa ya mama.

**TAASISI LISHE**

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TNFC) Dk. Germana Leyna, anasema takribani kuna vifo 823,000 vya watoto na 20,000 vya wanawake kila mwaka, wakati wa kujifungua duniani.

Dk. Leyna anasema, ni aina ya madhara yanayozuilika. Kutonyonyesha maziwa ya mama kwa mtoto, yanahusishwa na kuchangia kuwapo uwezo mdogo wa kiakili wa mtoto.

Mkuu huyo wa TFNC, anasema inasababishia hasara za kiuchumi kwa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 301 kwa mwaka, sawa Sh. bilioni 695.77 na Tanzania imechukua hatua mbalimbali kulinda unyonyeshaji maziwa ya mama.

Hapo anataja hatua hizo kuwa ni pamoja na upitishwaji kanuni kuu mbili zinazolenga kulinda muda wa mama kuweza kunyonyesha na kumlinda mama na jamii, vilevile ikiangalia suala la utoaji

elimu kwa jamii yote ya Kitanzania, itambue umuhimu wa unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa watoto.

"Jukumu kubwa la Taasisi ya Chakula na Lishe katika muktadha huu wa unyonyeshaji, ni kuhakikisha jamii inapata taarifa sahihi za lishe ikiwamo suala zima la uhamasishaji maziwa ya mama kwa mtoto, kupitia njia mbalimbali za upashaji habari," anasema Dk. Leyna.

Mkurugenzi huyo wa TFNC, ambaye pia ni mtaaluma wa fani ya afya, anatumia fursa ya hafla hiyo kumkaribisha Mama Modesta Kayuni, mnufaika wa kumnyonyesha mtoto maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya kwanza

Modesta, mkazi wa kata ya Mlowo, Mbozi hajawahi kuumwa tumbo kabisa na mtoto anaonyesha upeo mkubwa wa uelewa wa akili, hata analazimika kushukuru nyendo za serikali kwa wazazi wahitaji.

MAZINGIRA

UWEZESHAJI KUPITIA KILIMO;

# Mradi unaohamisha wasichana kutoka zahma isiyokoma ya kubeba mimba

## •Lengo kuwapa ujasiri kutetea haki zao

**Na Elizabeth Zaya**

ZIPO changamoto mbalimbali zimekuwa zikiwakwamisha wasichana kufikia malengo na ndoto zao hususani katika nchi zinazoendelea.

Takwimu za mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, ikiwamo la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), zinatamka umbali wa kwenda na kutoka shule, umekuwa ukichangia utoro na kusababisha mimba za utotoni kwa wasichana wadogo.

Nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa pamoja na wadau mbalimbali katika kufanikisha kutekeleza malengo ya maendeleo endelevu (SDGs), ikiwamo la nne linalohakikisha elimu kwa wote pamoja na usawa wa kijinsia, wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali za kumsaidia mtoto wa kike kuyafikia.

Msichana Initiative, ni miongoni mwa taasisi zisizo za kiserikali nchini zinazojikita kupambana kumsaidia mtoto wa kike kumpunguzia mzigo na changamoto zinazomkwamisha katika kutimiza malengo yake kwenye nyanja mbalimbali ikiwamo elimu pamoja na kufahamu haki zake nyinginezo.

Taasisi hii ya Msichana Initiative, imekuwa ikiendesha programu mbalimbali hususani za kumfikia moja kwa moja mtoto wa kike mahali alipo kumpatia elimu ya namna ya kutambua haki zake za msingi, lakini na kutoa misaada ya kufanikisha malengo yake pale inapowezekana.

Hivi karibuni, taasisi hiyo ya Msichana Initiative kwa kushirikiana na taasisi ya Sustainable Agriculture Tanzania (SAT) na ya PPIZ walizindua mradi mpya ambao unakusudia kukuza uwezeshaji wa wasichana wadogo kupitia kilimo, ambao unalenga pia kusaidia kupunguza tatizo la vitendo vya ukatili kwa wasichana hao.

Ni mradi uliopewa jina la 'Uwezeshaji Wasichana Kupitia Kilimo (GAPE)', ambao ni wa miaka miwili wenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 1.6 na unaotekelezwa katika mikoa ya Dodoma, Tabora na Zanzibar kwa ufadhili wa Ubalozi wa Ufaransa.



Msichana katika mradi wa kilimo akiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANADO.**

### KUTOKA KWA MKURUGENZI

Rebeca Gyumi ni Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, anasema mradi huo unatarajia kunufaisha wasichana 1000 waliochaguliwa katika mikoa hiyo miwili ya Dodoma na Tabora na wengine 1000 kutoka Zanzibar.

"Pia, mradi unalenga kujenga ujasiri kwa wasichana katika kutetea haki zao na kwa upande mwingine kuwapa mafunzo ya namna ya kuanzisha shughuli za kiuchumi hususani kwa kuanzisha kilimo Ikolojia, ambacho kinazingatia utunzaji wa mazingira na kuendelea kuhifadhi bioanuwai,"anasema.

Mkurugenzi huyo, anasema utafiti wa namna nyingi hivi karibuni, umebaini kwamba mapambano dhidi ya unyanyasaji kijinsia, ni lazima uambatane na uwezeshaji wanawake kiuchumi.

Katika hilo, anasema wao wameamua kuanzisha mradi huo, ili kuhakikisha kwamba wanapambana navyo kwa uwezeshaji wa wasichana hao kwa vitendo.

Rebeca anasema, walengwa watapangwa katika vikundi vya watu 35 vikijumuisha wanaume kwa asilimia tano, wenye umri kati ya miaka 15 na 35, ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli hizo na lengo kubwa mradi wa GAPE lengo lake kubwa ni kumsaidia msichana kuzifahamu haki zake na anazisimamia.

Anasema, mbali na mradi huo kumwezesha msichana kuzifahamu haki zake, pia unalenga kumwezesha kumuinua kiuchumi na pia ni njia ya kumuongezea nguvu ya kupaza sauti kuhusu namna ya kusimamia haki zake mbalimbali.

"Na mradi huu tunautekeleza kwa kipindi cha miaka miwili katika wilaya za Kongwa Dodoma na Nzega mkoani Tabora kwa Tanzania Bara, upo pia kwa Zanzibar," anasema Rebeca.

"Tumeamua kufanya mradi huu baada ya kuona changamoto ya ukatili wa kingono na kijinsia wanaopitia wasichana katika jamii tunazofanya nazo kazi, lakini wengi wao kukosa nguvu ya kufanya uamuzi kwa sababu ya utegemezi wa kiuchumi unaotokana na uhusiano usio sawa na wa kinguvu kwenye jamii yetu."

Rebeca anasema kwamba, wasichana hao watakaofikiwa watasaidia kuwaelimisha wenzao juu ya kutambua haki zao za msingi, pia namna ya kuendesha shughuli za kujikomboa kiuchumi.

"Na tunataka kupitia wasichana hawa tutakaowafikia wawe ni chachu ya kuleta mabadiliko kwa wenzao katika jamii zao hasusani kwenye kufahamu namna ya kutambua haki zao za msingi, na mradi huu utawafikia wasichana walio nje ya shule na hasa wale waliowahi kupitia ukatili au waliopata mimba za utotoni," anasema.

Mkurugenzi anafafanua kwa mfano: "Tuna mradi wetu mwingine unaojulikana kama 'Msichana mmoja, baiskeli moja' wa kuwapatia baiskeli wanafunzi wasichana wanaotembea umbali wa zaidi ya kilomita 10 kwenda kusaka elimu."

Anaendelea: "Kwa sababu, katika maeneo ambayo tumesaidia, kumeanza kuzaa matunda, ufaulu wa wasichana hao umeongezeka, kwa hiyo tunaamini na huu wa GAPE utaleta matunda."

Stephen Kiboko, ni Ofisa mradi kutoka 'Msichana Initiative' anasema kuna haja kubwa ya kulishirikisha kundi hili la wanawake na wasichana, katika shughuli za kiuchumi ikiwamo kilimo.

"Hii itasaidia kuongeza mapato kwenye jamii yetu, washirikishwe, pia katika michakato ya uamuzi inayofanywa iwe kwenye ngazi ya familia hadi kwenye mambo yenye ustawi wa taifa," anasema Kiboko.

Anasema mradi huo utasaidia kwa kiwango kikubwa kuongeza uzalishaji na hata kutatua changamoto, ambazo zimekuwa zikijitokeza kutokana na kukosekana kwa ushiriki wa wanawake na wasichana.

Joyce Joseph, kutoka Nzega, Tabora amepongeza taasisi hiyo ya Msichana Initiative na washirika wake kwa kuwaonyesha mwanga wasichana hususani kwa kuwawezesha kuanzisha biashara ndogo ikiwamo kilimo ikolojia.

"Mradi umekuja wakati mwafaka wakati wasichana na wanawake wengi bado tunajitahidi kupambana na mambo mengi ya ukatili ambayo yanaathiri maendeleo yetu.

"Kwa hiyo, uwezeshaji huu utatusaidia kuanza miradi ya kilimo ambayo pia inalenga utunzaji wa mazingira ya ikolojia na mazingira yetu asilia," anasema Joyce.

### WANUFAIKA & WANUFAISHAJI

Asha Emmanuel, ni miongoni mwa wanufaika, anasema mradi huo utawasaidia kujithamini na kufahamu mambo mengi ikiwamo haki zao za msingi kwenye jamii na itawaongezea ujasiri kupambana na kukemea vitendo vya ukatili dhidi yao na watu wengine kwenye jamii.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo Dar es Salaam hivi karibuni, Balozi wa Ufaransa Frederic Clavier, anasema mradi wa GAPE utatekelezwa ikiwa ni moja ya juhudi zinazofanywa na ubalozi huo kwa ajili ya kusaidia kuinua wanawake na wasichana pamoja na kuhamasisha utunzaji wa baioanuwai.

Clavier anasema, pia utasaidia kuongeza tija katika shughuli za kilimo kwa wanawake na kuimarisha usalama wa chakula katika jamii nufaika.



Rebeca Gyumi, Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, akiwa kazini.

MAZINGIRA

MAMBO MAPYA YA MRADI FORVAIC...

# Ulinzi misitu ulivyowaletea maisha mapya wakazi wa Namtumbo na mazingira yao

## •Neema kuanzia uchumi, kijamii, hadi...



Wajumbe wa Utawala Bora na Usimamizi wa Fedha wa Kamati za maliasili na viongozi wa kijiji wa Masuguru na Chengena, yaliyofanyika Namtumbo March 2021.**PICHA ZOTE: BEATRIECE PHILEMON.**

**Na Beatrice Philemon, aliyekuwa NAMTUMBO**

UKATAJI miti una athari. Lakini, unapowaambia wakazi wa wilayani Namtumbo Mkoa wa Ruvuma, leo hii hawako huko, wana hadithi yao. Kwa vipi?

Hivi sasa kuna Programu ya Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC) iliyoanza kuleta matokeo chanya kwa wananchi wake wameshaacha ukataji miti, iwe kwa kilimo au uchanaji mbao, katika misitu ya hifadhi vijijini.

Pia, hivi sasa wananchi hao wanaelewa namna ya kuhifadhi misitu wakiamini itawaletea fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo vijijini.

Hapo panatajwa vijiji vitano katika kata za Luchili na Limamu, chini ya Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Changomoto za Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USMJ).

**MKUTANO DARASA**

Mratibu wa Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Shabani Hamis, anasema FORVAC imeviwezesha vijiji vinne kutengeneza mfumo wa kieletroniki kufuatilia uhalifu misituni, huku mamlaka husika zikichukua hatua.

Programu FORVAC hadi sasa imewezesha kuhudumia misitu yenye hekta 22,900.88 za usimamizi shirikishi kwa vijiji vitano vilivyotengewa; Limamu, Kumbara, Kilangalanga, Chengena na Njalamatata.

Mratibu wa FORVAC Kongani ya Ruvuma, Marcel Mutunda, anasema programu inatekelezwa na Idara ya Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii, ikishirikiana na Shirika la Mpingo (MCDI), MJUMITA na Halmashauri ya Wilaya Natumbo.

Ni programu inayofadhiliwa na serikali ya Finland na Tanzania, lengo ni kuongeza faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira kutokana na usimamizi endelevu wa rasilimali misitu.

Hamisi anasema, hadi sasa MJUMITA imeshakiruhusu Kijiji cha Masuguru kuendelea na mpango wa matumizi bora ya ardhi, huku vingine vikipatiwa elimu ya utawala bora na usimamizi fedha.

Akizungumza katika warsha ya kuboresha utawala bora na usimamizi wa fedha katika usimamizi shirikishi wa misitu katika vijiji vine; Kilangalanga, Chengena, Limamu na Masuguru.

Hamisi anafafanua: " Wadau walifundishwa masuala ya uendelezaji wa biashara ya mazao ya misitu na mnyororo wa thamani, utawala bora na uraghabishi katika usimamizi wa misitu ya jamii."

Pia, anataja mengine ni usimamizi wa fedha, historia ya mradi FORVAC, mchango wa serikali katika uendelezaji wa usimamizi shirikishi wa misitu, fursa na magumu yaliyoko.

Hamisi anawataja walioshirikishwa wanajumuisha maofisa watendaji kata na vijiji, wenyeviti vijiji, madiwani kutoka kata husika na kamati za maliasili za maeneo hayo.

Ni mjumuiko wa viongozi 27 wa vijiji na kamati za maliasili za maeneo husika, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo.

Pia, FORVAC imeshaanzisha vikundi viwili vya kijamii katika kata za Luchili na Limamu, zenye vyombo vya kutetea na kudai haki, kiboresha uelewa wa utawala bora na kusimamia fedha.

"Lengo la mafunzo ni kusaidia viongozi wa vijiji ili yote yanayohusu misitu, uvunaji mbao, magogo, uuzaji, matumizi ya fedha yaamuliwe kwa kushirikisha wananchi kupitia mkutano mkuu wa kijiji.

"Pia, kuwapo uwazi katika mapato na matumizi, uwajibikaji na ushirikishwaji wananchi katika shughuli za uhifadhi wa misitu," anasema Hamisi .

Hadi sasa imeshatoa 'simu janja' (Smartphone) nne kwa wajumbe wa kamati za maliasili ili waweze kufuatilia uhalifu msituni na hivi sasa doria zimeimarishwa, zikiendeshwa na wajumbe wa kamati husika.

Vilevile, anasema wananchi wameshaanza kutoa taarifa za kasoro katika utawala bora wao, baada ya kupata mafunzo, hali iliyo tofauti na miaka ya nyuma.

Lingine linatajwa haja ya kuwapo nidhamu za uongozi wilayani, watendaji vijiji na wasio waaminifu na hadi sasa kuna vijiji vitano vya kata za Luchili na Limamu, ambavyo vimeshandaa mpango mkakati kukabiliana na magumu ya usimamizi shirikishi misituni.

**OFISA MJUMITA?**

Ofisa Uraghabishi na Mawasiliano wa MJUMITA, Revocatus Njau, anasema kutoka mwaka 2018 hadi sasa, kuna vikundi 10 vilivyoomba kufanya biashara ya mazao misituni.

Pia, inatajwa kijiji cha Limamu kilianzishwa mwaka 1974 na hadi kina wakazi 4,227 wenye kaya 625; kati yao wanaume 1835 na wanawake 2,392.

Hadi sasa kumeshatengwa msitu wa hifadhi wenye hekta 1784 na wameshaandaa mpango bora wa utumiaji ardhi uliokwishafunguliwa akaunti za kusimamia.

Hilo linaendana na kuundwa vikundi vya uzalishaji mali kama vile uchongaji, ufugaji nyuki na katika vikundi sita vilivyopo, vitatu vya useremala, viwili ufugaji nyuki na kimoja VICOBA.



Mratibu Mradi wa FORVAC Kanda Kusini, Shabani Hamis, akiwafundisha maofisa watendaji vijiji na kata, wenyekiti wao, madiwani na viongozi wa kamati za maliasili na viongozi wa vijiji vya Limamu, Chengena, Kilangalangana, Masuguru, kuhusu mradi ulivyo, elimu ya utawala bora na usimamizi wa fedha zake.

Rai yake ni kwa viongozi wa jiji, kata na madiwani kupiga marufuku uvunaji mazao misitu kwenye maeneo yasiyohifadhiwa na yaliyohifadhiwa, pia washirikiane kutunza misitu, ili wawaletee tija wakazi wanaozunguka misitu hiyo.

**UTAWALA BORA**

Hadi sasa inaelezwa viongozi wa kamati ya maliasili wa eneo husika wamefanikiwa kuripoti matukio mawili ya uhalifu misituni, ikiwamo utoaji alama za msitu.

Pia, Mhagama anasema wakosaji wanaokamatwa, hufikishwa kwenye ofisi ya kijiji kulipa faini na wanaoshindwa, hufikishwa kwa mamlaka za wilaya kwa hatua zaidi kisheria.

"Sisi kama kamati tuligundua watu hawa wakati tunafanya doria ndani ya msitu," anafafanua kuwa wengi wanajihusisha na ukataji miti ya mbao na wakulima kadhaa msituni Ndanje.

**MGAWANYO ARDHI**

Hadi sasa inaeleweka kijiji husika kimeshatenga ekari 22,000 za ardhi kilimo; ekari 11,000 za mifugo; na hekta 17841.43 za msitu kwa ajili ya usimamizi shirikishi, wakitarajia kuanza kuvuna Julai ijayo.

"Hivi sasa tupo kwenye hatua ya usimamizi na utunzaji wa msitu, doria, na tumepokea mashine ya kuchana mbao inayomilikiwa na wilaya za Songea, Namtumbo na Tunduru, mfadhili ni serikali ya Finland.

"Kabla ya mafunzo, uhalifu wa msitu uliyotokea uliathiri hekta tano kati ya hekta 17841.43 za msitu wa ndanje," anaongeza Mhagama, huku akifafanua wananchi wanajitolea kulinda msitu kwa ajili ya maendeleo ya kijiji.

Mhagama anasema, mfumo tajwa umesaidia kutuma taarifa ya uhalifu wa msitu kwa ufanisi wakimaliza wenyewe na taarifa iliyowafikia kupitia 'simu janja', matukio yaliyowafikia yanahusu uchanaji mbao, uanzishaji mashamba, kuchoma mkaa, alama za msitu, ulishaji mifugo msituni na kuchimba dawa kienyeji.

**CHANGAMOTO**

Anasema, hadi sasa wanakwamishwa na shida ya usafiri kutoka kijiji cha Limamu kufika msituni penye doria, pia wanakosa vifaa kazi na sare za kutekeleza jukumu lao.

"Tunakwenda kwenye doria na miguu, tunatumia saa 14 mpaka kufika kwenye msitu na njiani saa nyingine tunakutana na wanyama kama vile nyati, swala, tembo. Tunaomba msaada wa usafiri ili tuweze kufanya doria vizuri," anasema

Programu hiyo hadi sasa inatumika ndani ya mikoa ya Tanga, Dodoma, Lindi na Ruvuma katika wilaya ya Handeni, Kilindi, Mpwapwa, kiteto , Nachingwea, Ruangwa , Liwale, Songea, Namtumbo, Mbinga, Nyasa na Tunduru.

AFYA

CORONA KATIKA DALADALA...

# Kitendawili cha agizo RC Makalla kusuasua wasafiri na wasafirishaji

## •Chama cha Kutetea Abiria chaomba kusaidia

**Na Sabato Kasika**

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dar es Salaam, imetoa tamko la kusisitiza uvaaji barakoa kwa kila abiria wa mabasi ya umma na kuwataka wamiliki wa vyombo hivyo, kuwaelekeza madereva na makondakta kuepuka ubebaji abiria wasiovaa barakoa.

Ni hatua zilizochukuliwa kutokana na kinachoelezwa na Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla, kwamba kuna ulegevu wa usimamizi kwenye baadhi ya maeneo na anawaelekeza polisi, wakuu wa wilaya na Mamlaka ya Uthibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), kuhakikisha wanasimamia ipasavyo mwongozo wa serikali.

Katika kikao cha kamati hiyo kilichoketi juzi, kufanya mapitio ya tathmini ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa kuhusu kujikinga na corona, Mkuu wa Mkoa anaelekeza daladala kubeba wanafunzi watano watakaosimama, lakini kwa kigezo kwamba wawe wamevaa barakoa.

Pia, anasema wakae kwenye viti nikimanaisha 'level seat' anawataka wananchi kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, na kwamba ikitokea ulazima, taratibu zote za kujikinga na corona zinapaswa kuzingatiwa.



Abiria katika hali mchanganyiko, baadhi wamevaa barakoa na wengine hawajavaa.

### MWONGOZO ULIOPO

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeshatoa mwongozo mpya wa kudhibiti virusi vya corona, huku ikiagiza vyombo vya usafiri zikiwamo daladala kubeba abiria kulingana na idadi ya viti.

Mwongozo huo umetolewa kutokana na kuongezeka idadi ya wagonjwa wa corona ambao hadi wiki iliyopita, waziri mwenye dhamana, Dk. Dorothy Gwajima, anasema idadi ya waliombukizwa na kujulikana rasmi wamefikia 682, kutoka wastani wa wasiofika 200 si muda mrefu uliopita.

Kwa mujibu wa mwongozo, kila abiria kuvaa barakoa, kunawa maji tiririka na kutumia vitakasa mikono ni lazima, huku uongozi wa vituo vya mabasi ukitakiwa kusimamia uwapo wa vifaa hivyo.

Uongozi wa vituo vya mabasi nao unatakiwa kuhakikisha abiria wote wanavitumia vifaa hivyo, huku wamiliki wa magari ya abiria wakitakiwa kuweka vitakasa mikono katika vyombo hivyo na kusimamia uvaaji barakoa.

Wizara husika inataja kuwa maeneo yenye mikusanyiko ya watu, hasa ya huduma za kijamii, kibiashara, kiuchumi, kiofisi ni mojawapo ya vyanzo vya kusambaa kwa maambukizi ya corona katika jamii.

Yapo mengi ambayo mwongozo huo unaelekeza, ikiwamo kupiga marufuku mikusanyiko mikubwa ya kijamii kama sherehe, kisiasa na kidini isiyo ya lazima, ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii na hata kubadili tabia zao, wakizingatia mbinu za kujikinga na corona.

### HALI ILIVYO

Pamoja na kuwapo mwongozo huo, bado baadhi ya watu wamekuwa wagumu kuchukua tahadhari, hasa katika usafiri wa daladala jijini Dar es Salaam, ambayo Kamati ya Ulinzi na Usalama, imeamua kuingilia kati.

Hadi sasa katika uhalisia, Nipashe kupitia njia tofauti za daladala, imebaini hakuna mabadiliko kutokana na abiria kuendea kujaa ndani ya magari hayo, wengine wakishuhudiwa hawavai barakoa kana kwamba hakuna mwongozo huo.

Daladala kuendelea kujaza abiria kupita kiasi, wakati kukiwa na mwongozo, ni wazi kwamba ipo haja ya kutolewa elimu ya kudhibiti ugonjwa huo, pia viongozi husika wanafuatilia kujiridhisha iwapo mwongozo huo unazingatiwa.

Kitalamu ni njia inayoweza kuwasaidia Watanzania kubadilika, kufuatia na baadhi yao kutoona umuhimu wa kuzingatia mwongozo huo, badala yake wako tayari kujazana ndani ya daladala kuwahi katika shughuli zao.

Inawezekana sababu kubwa inayotawala ni ukosefu wa elimu au makusudi, hivyo hali ya mtindo wa viongozi kufuatilia kwa karibu ambacho wanaelekeza, unatajwa kuweza kuwa namna ya kusaidia kuifanya jamii ikabadilika na kuchukua tahadhari zote.

Ufuatiliaji unatajwa kusaidia kuibua mengi yanayochangia watu kujazana ndani ya daladala, kwani kuna wakati uhaba wa usafiri, inaweza kuwa chanzo cha hayo na kutafuta njia ya kumaliza tatizo bila kuathiri upande wowote.

Kwa kuwa LATRA wameshirikishwa, ni nafasi kwake kurudia walichofanya mwaka jana kwa kuruhusu magari mengine kusaidiana na mabasi ya mwendokasi na daladala, wasafirishe abiria wa jijini Dar es Salaam.

### KUTOLEWA ELIMU

Suala la kuepuka misongamano kwa kuzingatia umbali kati ya mtu mmoja na mwingine linatajwa kuwa na nafasi, huku kukirejewa ndani ya daladala, kunahitajika kutolewa elimu zaidi, hasa kushirikisha wadau mbalimbali.

Kwa mfano Chama Cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), kinasema kiko tayari kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kupitia Idara ya Afya, ili watoe elimu ya tahadhari ya ugonjwa wa corona ndani ya daladala.

Msemaji wa CHAKUA, Solomon Nkiggi, anasema kuna haja ya kutolewa elimu zaidi ndani ya usafiri huo wa umma, ili kuwasadia Watanzania kuwa makini dhidi ya ugonjwa huo.

"Suala la kuepuka misongamano kwa kuzingatia umbali kati ya mtu mmoja na mwingine ni la muhimu, lakini ndani ya daladala, kunahitajika kutolewa elimu zaidi, hasa kwa kushirikisha wadau mbalimbali," anasema Nkiggi.

Pia, anafafanua kwamba si daladala pekee, pia inagusa vyombo vingine vya usafiri jijini Dar es Salaam, lengo ni kuongeza nguvu zaidi baada kuona bado kuna uelewa mdogo kuhusu ugonjwa huo na kuna wasiochukua tahadhari sahihi.

"Suala la kuepuka misongamano kwa kuzingatia umbali kati ya mtu mmoja na mwingine ni muhimu, lakini ndani ya daladala, kunahitajika kutolewa elimu zaidi hasa kwa kushirikisha wadau mbalimbali," anaeleza.

Nkiggi anafafanua kuwa, viongozi wa chama chao wamekuwa wakizunguka ndani ya daladala na kushuhudia jinsi abiria wanavyojazana, na sasa wanaona kuna haja kushiriki kutoa elimu kwa abiria, kondakta na madereva.



Aina ya utaratibu unaoagizwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, katika vita kukabili Uviko 19. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



# HABARI DODOMA

## VETA yavisaidia vyuo vya ufundi

**Na Renataha Msungu,** DODOMA

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Kanda ya Kati, kimetoa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 62.8 kwa vyuo vya ufundi ambavyo havimilikiwi na mamlaka hiyo.

Aidha, fedha hizo ni sehemu ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo hutolewa kwa ajili ya kuinua kiwango cha elimu kwa mafundi mchundo na sanifu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Kati, John Mwanja, alisema kutokana na mchango wa elimu ya ufundi unaotolewa na vyuo hivyo, mamlaka imeona ni vyema viongezewe nguvu ili kuboresha ufundishaji ikiwamo kukuza uchumi wa taifa.

Mwanja pia alisema serikali inatoa fedha hizo kwa vyuo hivyo ili kudahili wanafunzi wengi zaidi ambao wakihitimu hupata fursa ya kujiajiri ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Vifaa vilivyotolewa katika vyuo vya ufundi vya Don Bosco, St. Gabriel na St. Ursula ni pamoja na vya umeme, ujenzi na ufundi,

kila chuo kimepewa kulingana na uhitaji wake.

Mwanja alisema serikali imekuwa ikitoa msaada huo kwa vyuo hivyo kwa awamu kutokana na bajeti iliyotengwa kwa mwaka husika. Awamu hii, vyuo vitatu vimepata huku vingine vitatu vya Sema VTC, Nangwa VTC na Veyula VTC viko katika hatua za mwisho za kupatiwa.

"Tunaomba vifaa hivi vikazidi kuchochea mafunzo ya ufundi vyuoni. Tunahitaji kuona wanafunzi wanaohitimu katika vyuo hivi hawana tofauti na wale wanaohitimu VETA," alisema Mwanja.

Pia alisema lengo lao ni kuona vijana wanapata elimu bora ambayo inaongeza usawa katika utoaji elimu ya ufundi hapa nchini.

Mkuu wa Chuo cha VETA Dodoma, Stanslaus Ntibala, alisema serikali iwakumbuke na wao katika ugawaji vifaa hivyo ili wazidi kutoa elimu bora kwa vijana wanaojiunga na vyuo hivyo.

Alisema vyuo hivyo vinavifaa lakini bado vinahitaji vya kisasa ili viweze kwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Sister Josephina Mboi, Mkuu wa Chuo cha St. Ursula, aliishukuru serikali kwa kuwapa vifaa hivyo huku akisisitiza chuo kitaendelea kutoa elimu bora ya ufundi kwa wanafunzi.

Alisema wanaishukuru VETA kutokana na ushirikiano wanaoutoa ili kuhakikisha vijana wanaohitimu katika vyuo hivyo wanakuwa sawa na wale wa mamlaka hiyo.

# Mkurugenzi abainisha kero sekta ya mifugo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Sera na Mipango katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Amos Zephania, amesema sekta ya mifugo bado inakabiliwa na matatizo mengi yakiwamo magonjwa kwa mifugo.

Zephania aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha salamu za Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, katika ufunguzi wa kongamano la saba la wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi kuhusu sera katika sekta hizo.

Alisema sekta ya mifugo nchini bado inakabiliwa na kero nyingi yakiwamo magonjwa ambayo yamekuwa yakiathiri kwa kiasi kikubwa mifugo nchini.

Kutokana na hali hiyo, alisema wizara inatoa wito kwa wadau mbalimbali kuwekeza katika kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa dawa za mifugo ili kukabili kero hiyo.

Aidha, alisema kero nyingine ni upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo hali ambayo imekuwa sababu kubwa inayoathiri sana sekta hiyo nchini.

"Wakati wa masika hata ng'ombe wale wa kienyeji utoaji wa maziwa unaongezeka. Lakini wakati wa kiangazi kiwango cha maziwa kinashuka na hii ni kutokana na uhaba wa maji pamoja na malisho ya mifugo. Nitoe wito kwa wadau kutafuta namna ya kuzalisha malisho," alisema Zephania.

Mkurugenzi huyo alisema pia kuna haja ya kuboresha mifugo inayozalishwa nchini ili kuendana na mahitaji ya sasa.

"Ng'ombe tulio nao hivi sasa nchini ni wadogo sana hawatoi maziwa ya kutosha, lakini hata nyama yao ni kidogo ambayo haiwezi kuleta ushindani katika soko, hivyo kuna haja kutafuta namna ya kuboresha mifugo hii," alisisitiza.

Kadhalika, alisema kero nyingine ni uhaba wa maofisa ugani nchini kwa kuwa wanaohitajika ni 17,000 na waliopo ni 3,397 ambao hawakidhi mahitaji.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kutokana na uhaba wa wagani, wizara imeamua kuanzisha mfumo wa M-Kilimo ambao utawawezesha wakulima kupata taarifa mbalimbali zitakazowasaidia kupata majibu ya maswali yao.

Pia alisema kuwa ili kuboresha mazingira na kuwezesha ukuaji wa sekta ya mifugo katika mwaka wa fedha 2020/21 wizara imeendelea kupitia sheria ya mifugo ambapo kanuni mpya nne zimeandaliwa na kutangazwa kwenye gazeti la serikali.



Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Lishe katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Grace Moshi, akiwasilisha mada kwenye warsha kwa waandishi wa habari kuhusu mwendelezo wa maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama Duniani, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Shia yawatoa hofu Watanzania kuhusu chanjo kujikinga corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JUMUIYA ya Shia Iman Ismail Muslims imewaomba Watanzania kutokuwa na hofu na chanjo inayotolewa bure na serikali kwa ajili ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya corona.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Kanda ya Kati, Nizar Bhanji, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari wakati wa uzinduzi wa chanjo uliofanyika jijini hapa.

Bhanji alisema Watanzania hawana haja ya kuwa na hofu na chanjo hiyo inayotolewa na serikali kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya corona badala yake wawe na imani kubwa kwa wataalamu huku pia wakimwomba Mungu.

Aidha, alisema serikali kupitia wataalamu wa afya wamefanya utafiti juu ya chanjo hiyo, hivyo Watanzania wanatakiwa kuhamasika kwa kujitokeza kwa wingi ili kushiriki kuchanjwa kwa kuwa ni muhimu katika kujikinga na ugonjwa huo.

"Ninawaomba Watanzania tuwe na imani kubwa na wataalamu wetu pamoja na serikali yetu hii ambayo iko chini ya mama yetu kipenzi Rais Samia Suluhu Hassan kuwa chanjo hii haina tatizo na ni vyema watu wote wakashiriki kwa hiari yao wenyewe," alisema.

Mwenyekiti huyo pia aliwashauri viongozi wa taasisi, mashirika na madhehebu ya dini kuendelea kutoa elimu ili kuwaondolea hofu waumini wao.

Alisema bado kuna umuhimu mkubwa kwa viongozi wa taasisi mbalimbali za kidini kuendelea kutoa elimu juu ya kushiriki kwa hiari kupata chanjo hiyo.

Naye Alkarim Saleh Mohamad, ambaye ni kiongozi wa jumuiya hiyo, aliwashauri viongozi wa jumuiya mbalimbali za kidini kutowapotosha Watanzania kuhusu chanjo inayotolewa.

Alisema wajibu wa viongozi hao ni kuwaelimisha waumini ili kwa wale wanaohitaji kupata chanjo hiyo waweze kushiriki kikamilifu, badala ya kujengewa hofu isiyo na tija.





# Mbeya yazindua kitabu cha mwongozo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umezindua kitabu cha Mwongozo wa Uwekezaji ambacho kimeainisha fursa mbalimbali za uwekezaji katika kila wilaya huku watendaji wa serikali katika ngazi mbalimbali mkoani humo wakitakiwa kushiriki kuzitangaza ili zifahamike.

Kitabu hicho kilizunduliwa juzi jijini hapa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ambaye alimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye alisitisha ziara yake ya siku sita ili kuwahi shughuli za kuaga mwili wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Elias Kwandikwa. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mwongozo huo, Prof. Ndalichako alisema Mkoa wa Mbeya una fursa nyingi za uwekezaji na kuwataka wananchi wa mkoa huo wakiwamo wafanyabiashara kuzitumia vizuri fursa hizo.

Aliwataka viongozi wa mkoa huo kuhakikisha wanashirikiana na wawekezaji ili kuondoa vikwazo vya kibiashara vinavyoweza kuibuka kwa lengo la kuwa na uwekezaji endelevu utakaoinua uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

"Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT), inaendelea kukabiliana na mdororo wa uchumi uliosababishwa na virusi vinavyosababisha ugonjwa wa corona ili benki zetu ziwe na uwezo wa kutoa mikopo mingi kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta mbalimbali, hivyo endeleeni kushawishi wawekezaji," alisema Prof. Ndalichako.

Alisema serikali inaendelea na ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa vya kuhifadhia mazao ili kukabiliana na tatizo la upotevu wa mazao baada ya kuvunwa ambao kwa sasa unakadiriwa kuwa kati ya asilimia 40 na 60 ya mazao ya wakulima yanapotea.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya aliwataka wawekezaji kuwekeza katika mkoa huo kwa maelezo kuwa kuna kila aina ya vivutio ikiwamo hali ya hewa nzuri inayovutia watu kutoka katika maeneo mbalimbali kuishi bila tatizo. Alisema Mkoa wa Mbeya una kila aina ya usafiri ambao unaweza ukawarahisishia wawekezaji kusafirisha bidhaa zao ikiwamo usafiri wa barabara na reli kwa kuwa mkoa huo unapitiwa na barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) pamoja na Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

Vilevile, alisema uwapo wa Uwanja wa Kimataifa wa Songwe (SIA) pia ni kivutio kingine cha uwekezaji kwa maelezo kuwa serikali kwa sasa inaendelea kuukarabati uwanja huo na kwa sasa kila aina ya ndege inaweza kutua.

Hata hivyo, alisema serikali imejenga meli za kisasa za mizigo na abiria katika Ziwa Nyasa ambazo zinarahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka Mbeya kwenda mikoa ya Njombe, Ruvuma na mikoa mingine ya Kusini pamoja na nchi jirani ya Malawi.

"Pia katika mkoa wetu kuna mawasiliano ya simu kila mahali, kuna huduma vituo vya kutolea huduma za afya kila mahali, tuna maji ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani na kwenye mashamba na zipo taasisi mbalimbali zinazosimamia uwekezaji," alisema Homera.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliitaka serikali mkoani Mbeya kulinda maeneo ya kilimo ili yasibadilishwe matumizi kama inavyotokea katika baadhi ya maeneo.

Alisema maeneo hayo yanaweza yakalindwa kwa kupimwa na kutolewa hatimiliki ili kuepusha wawekezaji kuanza kulazimika kuwalipa wananchi fidia wanapotaka kuwekeza.

Kaulimbiu ya uwekezaji katika Mkoa wa Mbeya inasema 'Wekeza Mbeya kwa Maendeleo endelevu'.



Mbunge wa Viti Maalum kupitia Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Bahati Ndingo (kulia), akikagua moja ya nguo zilizokuwa zikiuzwa na wajasiriamali wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Mwongozo wa Uwekezaji, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# SUA, NEMC waanzisha mradi utafiti madakio maji

**Na Ashton Balaigwa,** MBARALI

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wameanzisha mradi wa utafiti wa usimamizi endelevu wa madakio ya maji kupitia tathmini ya kuimarisha mtiririko wa maji kwa mazingira na utekelezaji wake katika kulinda Ukanda wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi kutokana na athari za shughuli za kibinadamu Tanzania (EFLOWS).

Mradi wa utafiti huo unalenga kuona masuala ya mazingira ya umwagiliaji, kilimo kando ya kingo za mito, ufugaji wa mifugo ndani ya kidakio cha mto Mbarali na Bonde la Rufiji na ongezeko la watu vinasimamiwa kwa uhifadhi kamilifu wa eneo la Magharibi mwa Ukanda wa Bahari ya Hindi.

Meneja Utafiti wa Mazingira kutoka NEMC, Rose Mtui, alisema hayo njini Mbarali, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa (NEMC), Mhandisi Dk. Samuel Mafwenga, wakati wa kumkaribisha mkuu wa wilaya hiyo, Reuben Mfume kuzindua mradi wa utafiti wa EFLOWS.

Mtui ambaye ni Mtafiti Mkuu mwenza wa mradi huo alisema, NEMC kwa kushirikiana na taasisi za kitaaluma, na za utafiti zimekuwa zikitengeneza miradi na kufanya utafiti ukiwamo huo ili kutatua matatizo mbalimbali ya kimazingira.

Mradi huo wa utafiti pia ni muhimu zaidi kwa ajili ya mtiririko endelevu wa maji kuelekea kwenye ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115 katika Mto Rufiji, mkoani Pwani.

"Mazingira na mifumo ya ikolojia na bioanuai zilizopo (nchi kavu na majini) na huduma zinazopatikana vinaendelea kupata changamoto kutokana na ongezeko la idadi ya watu, matumizi yasiyo endelevu, uchafuzi utokanao na kemikali," alisema Mtui.

Naye Mkurugenzi wa Masomo ya Shahada za juu utafiti uhauwilishaji wa teknolojia na ushauri wa kitaalamu wa Chuo Kikuu SUA, Prof. Esron Karimuribo, alisema upo uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji na upungufu wa maji yanayotiririka mtoni.

Pia, ubora hafifu wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na matokeo hayo yanayoonekana kwenye ikolojia nyingine za nchi kavu na maji.

# Huduma chanjo ya corona yazinduliwa rasmi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesema inakusudia kuzindua rasmi huduma ya chanjo dhidi ya ugonjwa wa corona kwa wananchi, uzinduzi ambao unatarajiwa kufanyika kesho katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa anahitimisha Mkutano wa Uzinduzi wa Kitabu cha Mwongozo wa Uwekezaji mkoani humo na aliwataka wananchi kujitokeza.

Alisema zoezi hilo litafanyika kwa bila gharama na kila anayetaka kuchanjwa atachanjwa bila kulazimishwa na itakuwa hiari na kwamba maelezo mengine wananchi watapatiwa na wataalamu wa afya.

"Natangaza kwamba Ijumaa itakuwa ni siku ya uzinduzi rasmi wa chanjo ya corona katika Hospitali yetu ya Rufani ya Mbeya, kwa hiyo nawaomba wananchi tukutane pale kwa wale ambao wanataka," alisema Homera.

Awali, wakati akiwa ziarani mkoani Mbeya, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwataka wananchi kuwapuuza watu wote wanaopotosha taarifa za chanjo hiyo na badala yake kila anayetaka akachanjwe kwa hiari yake.

Alisema serikali imeweka utaratibu mzuri wa kuchanja chanjo hiyo bila kulazimishana na chanjo hiyo imethibitishwa kuwa ni bora na haina shida yoyote kama baadhi ya watu wanavyoamini.

"Hakuna Mtanzania yeyote ambaye atachanjwa bila hiari yake, sasa sisi tunatoa wito kwa Watanzania wote kujitokeza kwenye vituo vilivyoainishwa ili wakachanjwe," alisema Majaliwa.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo kwa kuepuka misongamano, kutosalimiana mikononi, kuvaa barakoa na kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka mara kwa mara au kutumia vitakasa mikono.



HABARI ZANZIBAR

# Walalamikia kushamiri kwa vitendo vya uhalifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wa Shehia ya Kilimahewa wamelalamikia vitendo vya uhalifu vikiwamo uporaji na ukabaji wa kutumia mapanga vilivyoshamiri katika eneo hilo.

Walitoa malalamiko hayo jana kwa uongozi wa serikali ya mkoa wa Mjini Magharibi katika mkutano maalumu uliofanyika katika viwanja vya CCM Mkoa, Amani Mjini Unguja kwa shehia za Amani, Kilimahewa Juu, Kilimahehwa Bondeni, uliowashirikisha viongozi na watendaji mbalimbali wa mkoa huo.

Walisema pamoja na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na uongozi wa shehia katika kupambana na vitendo hivyo ikiwamo kuanzisha vikundi vya polisi shirikishi jamii, bado hali hairidhishi.

"Kwa kweli vitendo vya uhalifu wa kutumia mapanga na unyang'anyi vimeshamiri katika mitaa yetu. Tumekuwa hatuna amani vijana wamekuwa wakikaba asubuhi bila woga. Pamoja na jitihada ya kuwapo polisi jamii matukio hayo yanafanyika," alisema Ali Khamis, mmoja wa wananchi hao.

Pia alieleza kusikitishwa kwao na hatua ya Jeshi la Polisi kuwapatia askari maalumu wa shehia ambaye hana uwezo wa uwajibikaji katika shughuli za shehia kwa sababu mbalimbali ikiwamo suala la afya zao kutokuwa nzuri.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa katika hili hapa tuseme wazi bila ya kificho wenzetu wa Jeshi la Polisi baadhi ya askari wanaotuletea katika shehia hawafai kabisa. Uwajibikaji wao hauleti ufanisi maana wagonjwa. Inaweza kufika miezi mitatu askari hajafika katika shehia, tukiuliza tunaambiwa mgonjwa," alisema.

Pia wananchi hao walielezea tatizo la uhamiaji holela usiofuata utaratibu katika shehia zao hatua ambayo imekuwa ikiongeza changamoto mbalimbali hasa pale wananchi wanapopata tatizo.

Akijibu kero hizo, Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, aliwaagiza masheha na wananchi wa shehia hizo kuwafichua vijana wanaojihusisha na vitendo vya kihalifu ili serikali iwachukulie hatua.

"Tumekuwa tukipata malalamiko mengi kuhusu vitendo hivi vya uhalifu wa vijana wetu kutumia mapanga, kukaba na kunyang'anya watu. Sasa agizo langu masheha tuleteeni majina tupate kuchukua hatua," aliagiza Kitwana.

Mkuu wa Mkoa huyo pia aliwataka masheha kushirikiana na wasaidizi wao kuwatambua wananchi wanaoingia na kutoka katika shehia zao na kuhakikisha kila anayeingia anakuja na barua ya eneo analotoka.

Kuhusu ajira kwa vijana, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka, alisema pamoja na juhudi kubwa zinazochuliwa na serikali ya mkoa kwa kushirikiana na wilaya kulitatua tatizo hilo, bado utayari na uwezo wa vijana wengi katika kutumia fursa za ajira zilizopo ni mdogo.

"Tumekuwa tukichukua jitihada mbalimbali kutafuta fursa za ajira kwa vijana wetu na wafadhili tunao. Kama sasa hivi wenzetu wa uongozi wa NMB wapo tayari kutupatia boti 50 zilizokamilika vifaa vyote, lakini vijana wenye uwezo wa kuzitumia hatujawapata," alisema Msaraka.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipokea hati ya utambulisho kutoka kwa Balozi Mdogo wa Msumbiji anayefanyia kazi zake Zanzibar, Agostino Abacar Trinta, Ikulu Mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Ataka kasi ya kupambana na dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Abdalla, amewataka watendaji wa mkoa huo vikiwamo vyombo vya ulinzi, kupambana na kasi ya dawa za kulevya kwa sababu wasafirishaji wanatumia bandari bubu zipatazo 34.

Abdalla alisema hayo jana wakati akizungumza na watendaji wa mkoa huko Tunguu ikiwa ni mkutano wa kufanya tathmini ya utendaji katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mkuu huyo alizitaja changamoto kubwa za kasi hiyo kuwa ni pamoja na kuwapo kwa bandari bubu ambazo zinatumiwa na watu wenye nia mbaya kuingiza na kusafirisha dawa za kulevya.

Aidha alisema kuwapo kwa harakati nyingi za shughuli za uwekezaji wa hoteli za kitalii kwa kiasi kikubwa nako kumechangia na kuwafanya vijana kujishughulisha na biashara hiyo.

"Hizo ndizo sababu kubwa za kuwapo kwa kasi ya matumizi ya biashara ya dawa za kulevya katika mkoa wa Kusini Unguja. Tunakusudia kuweka mikakati zaidi katika kudhibiti maeneo hayo," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Suleiman Hassan, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano zaidi kuhusu taarifa za matukio ya dawa za kulevya na kuyafikisha katika vyombo vya sheria.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantum Haji Dau, alivitaka vyombo vya sheria na vile vya dola kuwakamata watuhumiwa wanaofanya biashara ya dawa za kulevya na kuwanyima dhamana.

"Tunaviomba vyombo vya sheria kuwanyima dhamana watuhumiwa wanaokamatwa na dawa za kulevya kwa sababu serikali imefuta dhamana kwa watuhumiwa wa aina hiyo," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Kudhibiti na Kuratibu Dawa ya Kulevya, Luteni Kanali Burhani Zubeir, alisema mafanikio ya kupambana na dawa za kulevya yapo kwa vyombo vya sheria ambavyo vitatoa taarifa kwa wananchi kuhusu matukio hayo.

# Waziri ataka wanandoa kuwa na subira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Abdalla Hussein Kombo, amewataka wahitimu wa mafunzo ya ndoa kuitumia elimu hiyo kwa kujenga subira na uvumilivu ili kudumisha ndoa zao.

Aliyasema hayo jana katika ukumbi wa Msikiti wa Jaamiu Zinjibar Mazizini wakati akikabidhi vyeti kwa wahitimu wa mafunzo ya ndoa.

Kombo alisema lengo la kupatiwa mafunzo hayo kwa wanandoa ni kuwa walimu kwa wengine na kujenga imani, subira na uvumilivu katika ndoa zao.

"Dawa pekee ya kudumisha ndoa ni kuwa na subira hasa kwa wanaume ingawa changamoto kubwa ni kinamama kukosa uvumilivu," alisema Waziri Kombo.

Aidha, alisema dini imetoa miongozo mbalimbali ya kisheria kwa lengo ya kuitunza ndoa na kuipa hadhi na heshima yake kwa kubainisha haki na wajibu kwa wanandoa.

Naye Katibu wa Mufti, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema ameridhishwa na mwamko wa wanafunzi wanaohitaji elimu ya ndoa jambo ambalo litasaidia kuepusha wimbi la talaka.

Alisema mafunzo mbalimbali waliyoyapata wahitimu hao ni pamoja na maana ya ndoa kisheria, uchaguaji wa mchumba, nafasi ya wazazi kwa wanandoa pamoja na sifa za familia.

Mfaume alisema kuwa licha ya mafunzo hayo wahitimu hao pia wamefahamishwa viashiria vya migogoro katika ndoa na matokeo ya migogoro hiyo.

Kwa upande wao, wahitimu hao waliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Mufti kwa kuwapatia mafunzo hayo bila ya malipo ambayo yatasaidia kuimarisha ndoa zao.

Watu 195 wamehitimu mafunzo hayo ambayo ni awamu ya 10 tangu yalipoanza kutolewa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**

**SHAURI LA LUFAA YA JINAI NAMBA 31 YA 2021**

**ZUHURA KHERI JUMA........MKATA RUFAA**

**DHIDI YA**

**ABDALLAH RAJABU........MRUFANIWA**

**KWA ABDALLAH RAJABU**

**KUITWA SHAURINI**

Kwakuwa mleta rufaa ameleta rufaa yake ambayo maelekezo yake yameelezwa katika nakala za rufaa ambazo zinaweza kupatikana katika mahaka hii,kwa hiyo unahitajika kuhudhuria mahakama hii binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya jumatano tarehe 8 mwezi 9 mwaka 2021 saa 2:00 asubuhi

Kwa mujibu wa rufaa hiyo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika katika shauri hilo

**ANGALIZO**

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitika kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa

Hati hii imtolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 4 mwezi 8 mwaka 2021.

116392101

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARI HAMISI BINDE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **MITSUBISHI PICK-UP** yenye namba za usajili **T 815 BHE.** Chasis No. **FE638E502089,** Engine No **4D35585544** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/ RB/381865/2021.**

116392202

## KUPOTELEWA NA CHETI



KATIBU MKUU WA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA (KKKT) DAYOSISI YA KASKAZINI MAGHARIBI, ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA CHUO CHA NDUGU **GEOFREY NATANARY NGUVILWE** CHENYE NAMBA **JK200092,** ALIYESAJILIWA NA CHUO KIKUU CHA JOSIAH KIBIRA -BUKOBA MWAKA 2013 KWA NAMBA **JK/BAED/2013/0143** NA KUHITIMU MWAKA 2016.

AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA NAMBA **MBE/TUK/RB/706813/2020,** KWA YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KATIKA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU APIGE SIMU NAMBA **0768761001 AU 0767909015.**

116392502

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT COURT OF ILEMELA DISTRICT AT ILEMELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 7 OF 2021**

**In the matter of the estate of the late FR. PASCHAL IZENGO**

**AND**

**In the matter of Application for Grant of Letter of Administration by FR JOSEPH NCHORE**

**GENERAL CITATION**
**{RULE 75}**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant for letters of and probate and Administration is made to the above named petitioner

Caveat/ object to the grant should be filed on or before 20th day of August 2021.

Dated at Mwanza this 19th day of July, 2021.

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
ILEMELA – MWANZA.

116392602

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.229/2021**

**Ombi la MARY MSHITA TARIMO & ANNA PETER EMANUEL Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu PETER EMANUEL KAVISHE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 15/09/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 02/08/2021

116392702

## KUPOTEA KWA CHETI



**BARNABA NTANDU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0150/0011** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary SAME mwaka 2010,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **SIN/SIN/RB/382795/2021**

116392802

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.233/2021**

Ombi la **REHEMA RAJAB BANGO** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **HABIBA ATHUMAN BANGO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 23/08/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 03/08/2021**

116392902

## KUPOTELEWA NA CHETI



**CHRISTOPHER MWITA RYOBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S.11880054** KILICHOTOLEWA MWAKA 2013 NA BARAZA LA MITIHANI TANZANIA KUPITIA SHULE YA SEKONDARI NELUKA.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/634215/2021**

116393002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DONATILA MECKSON MCHAPE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya ISUZU JOURNEY lenyen namba za usajili **T 925 DKR** chasis namba **LR212J3000184** engine namba **6BG1EAA0184,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **MKB/TR/RB/139/2021**

116393302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BETH LWIDIKO MCHAPE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MITSUBISHI BUS lenye namba za usajili **T 655 DJA** chasis namba **MK516J20089** engine namba **677472,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **MKB/TR/RB/139/2021**

116393402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Mgodi wa kuchenjua dhahabu wa **Buckreef** uliopo Lwamgasa Mkoani Geita unatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **Toyota Landcruiser** Single Cabin nyeupe yenye namba za usajili **T329 DWD** lenye Chassis namba **JTELB71J90B010288** Engine namba **1HZ0940675.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye. Taarifa ya Polisi **RB REF/GE/TR/RB/ 182/2021**

116392302

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMILIANAROSE LUCAS MAHUNDI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4624/0008** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia PREMIER GIRLS SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/KIL/RB/337219/2021.**

116393502

## KUPOTEA KWA VYETI



**HENRICK E. DASTAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4645/0015** kilichotolewa na MWANZA ALLIANCE SEKONDARI mwaka 2008. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/381935/2021.**

116393102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**katika Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Wilaya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 93/2021**
**MDAI JAMES OBEID**
**DHIDI YA**
**MDAIWA PATRICK MAZENGO**
**KWA PATRICK MAZENGO**
**CHADULU**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba **MADAI YA PESA Tsh. 1,720,000/=.**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya **JUMANNE tarehe 10/08/2021 saa 2:30** asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 02/08/2021.**

116393802

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO.70. 2021**

**In the matter of the Estate of the LATE BORN MALRMILE MALASO of CHINYOYA within Dodoma city**
**And**

**In the matter of the Application for letters of Administration by**
**YONA CHRISTOPHA BORN**
**MALASO.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 25TH day of AUG 2021

**Dated at Dodoma this 03RD day of AUGUST 2020**

RESIDENT MAGISTRATE
.....................................
**DODOMA**

116394002

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Watu wanne wauawa, 20 wajeruhiwa

**KABUL,** AFGHANISTAN

WATU wanne wameuawa na wengine 20 wamejeruhiwa kwenye mashambulizi ya kupanga ya mabomu na bunduki yaliyomlenga waziri wa ulinzi na wabunge kadhaa katika mji mkuu wa Afghanistan Kabul.

Iliripotiwa jana kuwa bomu la kwanza lililipuka katikati mwa Kabul, Jumanne jioni na kusababisha moshi mzito kutanda katika anga la mji huo.

Waziri wa ulinzi Bismillah Mohammadi alisema lilikuwa shambulizi la bomu la kutegwa kwenye gari lililofanywa na mshambuliaji wa kujitoa muhanga lililoilenga nyumba yake na baadhi ya walinzi wake walijeruhiwa.

"Kabla ya masaa mawili kupita, milipuko mwingine ulifuatiwa na milipuko midogo na milio ya risasi iliyoutikisa mji wa Kabul karibu na eneo lenye ulinzi mkali la (Green Zone), ambako ni makazi ya balozi kadhaa ukiwemo ubalozi wa Marekani," alisema.

Aliongeza kuwa hakuna kundi lililodai kuhusika na hujuma hiyo, lakini Marekani inalinyooshea kidole cha lawama kundi la Taliban.

**DW**

# Japan kubadili sera yenye utata wagonjwa kulazwa hospitalini

**TOKYO,** JAPAN

WAZIRI wa Afya wa Japan amesema, kwamba serikali imepanga kufikiria kugeuza sera mpya yenye utata inayowataka wagonjwa wa COVID-19 wasio na dalili kali za ugonjwa huo, kujiweka karantini badala ya kwenda hospitalini. Mwanzoni mwa wiki hii, Waziri Mkuu wa Japan Yoshihide Suga alitangaza kwamba wagonjwa mahututi wa COVID-19 wanaohitaji msaada wa kupumua au ambao wanaweza kuwa na dalili kali za ugonjwa huo ndio watakaolazwa hospitalini.

Waziri wa Afya Norihisa Tamura alitetea sera hiyo, akisema kwamba kwa kuwataka wagonjwa wasio na dalili kali za COVID-19 kujitenga, Japan inaweza kuhakikisha kuwa hakuna uhaba wa vitanda katika hospitali mbalimbali kwa watu wanaohitaji uangalizi mkubwa.

"Janga hilo limeingia katika hatua mpya na kama hatutakuwa na vitanda vya kutosha, hatuwezi kupokea wagonjwa zaidi hospitalini, na ikiwa mambo hayataenda kama ilivyopangwa, tunaweza kupitia sera hii," alisema Tamura akiwa analihutubia Bunge.

Aliongeza, huku akibaini kuwa mabadiliko hayo ya sera yanalenga kudhibiti kuenea kwa haraka kwa aina mpya ya kirusi cha Corona, Delta.

**RFI**

# Rais Macron kuchangisha fedha kuisaidia Lebanon

**PARIS,** UFARANSA

RAIS wa Ufaransa Emmanuel Macron anatarajia kukusanya zaidi ya dola milioni 350, euro milioni 295, ili kuisaidia Lebanon wakati wa mkutano ulioandaliwa kusaidia raia wa Lebanon, mwaka mmoja baada ya mlipuko wa bandari ya Beirut.

Mwaka mmoja baada ya mlipuko ulioharibu bandari ya mji mkuu na kuitumbukiza Lebanon katika mgogoro mkubwa wa kiuchumi, viongozi wake wa kisiasa bado wameshindwa kuunda serikali, licha ya shinikizo la Ufaransa na kimataifa. "Kadiri hali inavyoendelea kuzorota, hitaji la serikali linazidi kuwa la haraka zaidi," mshauri wa Rais Macron aliwaambia waandishi wa habari.

Ufaransa imeongoza juhudi za kimataifa, ili kuondoa koloni lake la zamani katika mgogoro huo. Rais Macron ambaye alizuru mji wa Beirut mara mbili tangu kutokea kwa mlipuko huo, alitoa msaada wa dharura na kuchukua hatua za kuzuia kuingia nchini Ufaransa maafisa wa Lebanon, ili nchi hiyo iweze kuweka mpango wa mageuzi.

Ameshawishi pia Umoja wa Ulaya kukubaliana juu ya mfumo wa vikwazo ulio tayari kutumika.

Lakini, mipango yake ikiwa ni pamoja na kupata ahadi kutoka kwa wanasiasa wa Lebanon kukubaliana juu ya kuwekwa kwa serikali ya mageuzi, bado haijafanikiwa.

Rais wa Marekani Joe Biden atahudhuria mkutano huo, ambao unaandaliwa kwa ushirikiano na Umoja wa Mataifa, ofisi ya rais wa Ufaransa imesema, Viongozi 40 duniani, ikiwa ni pamoja na rais wa Misri, kiongozi wa Jordan, Iraq na Canada watashiriki mkutano huo, na Uingereza kuwakilishwa na waziri wake wa mambo ya nje.

Mwaka jana, mkutano uliofanyika baada ya mlipuko ulikusanya karibu dola milioni 280.

Ofisi ya Rais Macron ilisema, msaada huo mpya wa kibinadamu hautakuwa na masharti yoyote, lakini karibu dola bilioni 11 zilizokusanywa mwaka 2018, bado zinazuiliwa kwa masharti ya mageuzi kadhaa yatakayotekelezwa na viongozi wa kisiasa.

**RFI**



Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron (katikati), akiwa ziarani Lebanon baada ya Bandari ya Beirut kuharibiwa na mlipuko wa bomu. **Picha AFP**

# Ahukumiwa kifungo, kulipishwa faini baada ya kukutwa na kifaru

**BERLIN,** UJERUMANI

MSTAAFU mmoja nchini Ujerumani ametiwa hatiani kwa kosa la kumiliki silaha baada ya kubainika kuwa na silaha kubwa binafsi kikiwemo kifaru kinachodaiwa kuwa kilitumika katika vita ya pili ya dunia.

Kwa mujibu wa ripoti ya BBC iliyosambazwa jana ilieleza kuwa, mtuhumiwa huyo mwenye umri wa miaka 84, alihukumiwa kifungo cha miezi 14 na kuamriwa kulipa faini ya pauni 213,469.

Maafisa nchini humo walibaini kuwepo kwa kifaru na vifaa vingine vya kijeshi vya enzi ya vita vya pili ya dunia, kwenye makazi ya mzee huyo katika mji wa Heikendorf mwaka 2015.

Mwanzoni mwa wiki hii, mahakama nchini humo iliamuru kuwa mtuhumiwa huyo ambaye jina lake halikutajwa, kwa sababu ya sheria ya faragha ya Ujerumani, lazima auze au akigawe kifaru hicho na silaha ya kupambana na mashambulizi ya anga iwekwe kwenye makumbusho.

Kwa mujibu wa wakili wa mtuhumiwa, alibainisha kwamba idara ya makumbusho ya Marekani ina nia ya kununua kifaru hicho.

Wanahistoria wengi wa Marekani walisema kilikuwa kifaa bora zaidi kilichotumiwa na Ujerumani wakati wa vita vya pili vya dunia.

Vyombo vya habari vya nchini humo viliripoti kuwa, mwanasheria huyo alibainisha kuwa, maafisa wanaokusanya vifaa vya kijeshi vya Ujerumani walitaka silaha nyingine kama vile bunduki na bastola zilizotumika enzi hizo.

"Mamlaka za mji huo zilivamia makazi yake mwaka 2015 baada yakupata taarifa kuhusu vitu vinavyomilikiwa na mstaafu huyo, taarifa hiyo ilitolewa na wafanyakazi wenzao wa Berlin, ambao awali walifanya upekuzinyumbani kwake wakitafuta mchoro ulioibiwa baada ya enzi za Nazi," alisema.

Pia, iliripotiwa kuwa wanajeshi zaidi ya 20 walitumia zaidi ya saa tisa, kukiondoa kifaru hicho kutoka kwenye makazi ya mstaafu huyo. Vyombo vya habari vya nchini humo viliripoti kwamba mtu huyo aliwahi kuonekana wakati mmoja wa baridi kali akitumia kifaru kama jembe la kuondolea barafu.

**BBC**




# MBAPPE
## AENDELEA KUJIWEKA MTEGONI

**MANCHESTER, England**

KYLIAN Mbappe amekuwa akisuasua kufanya uamuzi wa kusaini mkataba mpya klabuni Paris Saint Germain, akihusishwa na dili la uhamisho kwenda Real Madrid, klabu aliyowahi kuitaja kama ndoto yake ya udogoni.

Nyota huyu amekuwa kwenye rada ya Real Madrid kwa muda, lakini inaonekana bado wataendelea kuwa mawindoni tu.

Kulikuwa na habari kuwa Mbappe angeuzwa katika msimu huu wa uhamisho, kwa sababu klabu hiyo inahofia kumpoteza bure au kwa hasara uhamisho ujao.

Taarifa kutoka PSG zinasema kuwa Mbappe atamalizia muda wake uliobakia kwenye mkataba wake na PSG.

Nyota huyo anatambulika kuwa hakuwa na mpango wa kulazimisha kuondoka mapema klabuni hapo, na taarifa zinasema ameamua kuwa atamaliza mkataba wake, bila kuongeza mda klabuni hapo.

Licha ya ukweli kuwa Mbappe bado hashawishiki bado kuongeza mkataba PSG, hii haiwahakikishii Real Madrid kuwa wapo katika nafasi nzuri ya kumpata nyota huyo, kwa sababu lolote linaweza kutokea.

# ATLETICO KUMKOSA JOAO UFUNGUZI LALIGA

**MADRID,Hispania**

KLABU ya Atletico Madrid itaanza kutetea taji lake la Ligi Kuu Hispania, LaLiga bila nyota wao, Joao Felix.

Felix alikuwa ni sehemu muhimu ya kikosi cha Atletico kilichotwaa taji la LaLiga msimu uliopita.



Nyota huyo atashindwa kushiriki kwenye mwanzo wa utetezi wa taji wa kikosi cha Diego Simeone, kutokana na kuuguza majeruhi.

Nyota huyo raia wa Ureno alishiriki michuano ya Euro 2020 akiwa na mamuivu ya enka na akalazimika kufanyiwa upasuaji kutokana na tatizo hilo.

Taarifa zinadai bado haifahamiki Felix atarejea lini dimbani, lakini inatarajiwa tarehe ya kurejea kwake itakuwa Septemba akifuatiliwa kwa ukaribu hali yake na mtaalamu, Cornelis Nicolaas Van Dijk.

Kwa sasa nyota huyo mwenye thamani ya karibu euro milioni 100 anatajwa anaelekea poa kurejea dimbani, lakini atahitaji kusubiri.

Atletico Madrid wanatarajia kukutana na Celta Vigo na Villarreal, mechi ambazo Felix atazikosa kwa kipindi anachouguza jeraha lake la enka.

# MADRID YAWEKA MASHARTI KWA ODEGAARD

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid wanadaiwa wanataka kuwekwa kwa kipengele cha kumnunua tena nyota wao Martin Odegaard kwenye klabu yoyote atakayoenda msimu huu wa joto.



Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 alikuwapo Arsenal kwa mkopo, na washika bunduki hao wanataka kuhakikisha wanamchukua kwa mkataba wa kudumu.

Kocha mpya wa Real Madrid, Carlo Ancelotti anadaiwa kumwambia Odegaard hawezi kumhakikishia kuanza nafasi ya mara kwa mara dimbani, hivyo kuondoka Santiago Bernabeu kunaweza kuwa ni fursa yake ya kupata mechi zaidi.

Odegaard anajaribu kupima machaguo aliyonayo, na anaaminika yupo tayari kurejea Arsenal licha ya klabu hiyo kukosa kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 25.

Real Madrid wapo tayari kupokea ofa ya pauni milioni 42.7, ili kumwachia nyota huyo aondoke, lakini klabu hii inasisitiza kuwa inahitaji kuwepo na kipengele cha kuwawezesha kumnunua tena ikiwa watamhitaji baadaye.

Nyota huyo amecheza mechi 20 msimu uliopita akiwa na Arsenal, akifanikiwa kufunga mabao mawili na asisti mbili kwenye mashindano yote.



# INTER
## YAKATAA KUMUUZA LUKAKU

**MILAN, Italia**

BINGWA wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Inter Milan imekataa ombi la klabu ya Chelsea kumnunua mshambuliaji, Romelu Lukaku kwa pauni milioni 85.

Lukaku mwenye umri wa miaka 28 anawaniwa na Chelsea inayotafuta mshambuliaji mpya baada ya Borussia Dortmund kukataa kumuuza straika wake, Erling Braut Haaland msimu huu wa majira ya joto.

Mbelgiji huyo aliyewahi kucheza Chelsea, alikuwa mtu muhimu msimu uliopita wakati Inter Milan ilipotshinda taji la kwanza la Serie A tangu mwaka 2010.

Ripoti zimesema Chelsea ilikuwa inakusudia kumjumuisha beki wa Mhispania Marcos Alonso, kwenye dili hilo la usajili wa Lukaku.


Haijafahamika iwapo bingwa huyo wa Ligi ya Mabingwa ulaya itaongeza ofa, ingawa Inter inaamini inaweza kukataa ofa hiyo na wakati uliopita Lukaku aliwahi kusikika akielezea nia yake ya kubaki klabu hiyo ya Italia.

# CITY YAJITOSA KUMSAJILI BOTMAN

**MANCHESTER, England**

BINGWA wa Ligi Kuu England Manchester City imeripotiwa kumfuatilia beki wa Lille ya Ufaransa, Sven Botman baada ya mlinzi huyo wa kati kuzivutia Liverpool na Manchester United.

Botman alikuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Lille, msimu uliopita na alishiriki kikamilifu kuisadia timu yake kuifunga Paris Saint-Germain hadi kubeba ubingwa wa Ufaransa, Ligue 1.




Beki huyo mwenye umri wa miaka 21 amehusishwa kuhamia klabu kadhaa za Ligi Kuu England msimu huu zikiamo Liverpool, Manchester United, West Ham na Newcastle.

Lakini, gazeti la L'Equipe la Ufaransa limeripoti kuwa City, pia inamfuatilia raia huyo wa Uholanzi baada ya kutahadharishwa anaweza kuhama msimu huu.

Ripoti zaidi zimesema Lille itataka ada ya pauni milioni 43 kumnunua beki huyo wa kati anayechipukia.

Botman alitia saini mkataba wa miaka mitano na Lille baada ya kujiunga na klabu hiyo msimu uliopita akitokea Ajax ya

# GREALISH AREJEA MAZOEZINI VILLA

**LONDON, England**

KLABU ya Aston Villa tayari wamemkaribisha Jack Grealish mazoezini wakati nyota huyo akihusishwa zaidi na uhamisho wa kwenda Manchester City.

Nyota huyu amefurahia likizo ndefu baada ya kukamilisha kibarua chake kwenye Euro 2020, huku chini ya kapeti kukiwa na habari za nia za timu za Ligi Kuu England (EPL), kuiwinda saini yake.

Villa wanatajwa kuwa tayari kupokea ofa ya pauni milioni 100, kwa ajili ya uhamisho wa nyota huyo.

Kupitia ukurasa wa Twitter wa Aston Villa wameonyesha Grealish akiungana na kikosi cha kwanza, kwenye mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya.

Taarifa zinasema mamlaka za klabu zinaendelea kuangalia namna ya kushughulikia suala la mchezaji huyo wakiamini wanaweza kumshawishi asalie kwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki.

Wakati huo huo City wanatarajia Grealish awasilishe ombi la uhamisho klabuni hapo.



HABARI MICHEZO

## KWA UFUPI

### KANE AKARIBIA CITY
MANCHESTER City wako tayari kulipa pauni milioni 130 kwa ajili ya mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, na wamesalia na matumaini kwamba wanaweza kusaini mkataba naye. ***(Athletic)***

### MADDISON MAMBO SAFI
ARSENAL wamependekeza mkataba wa nyongeza ya fedha kwa ajili ya kiungo wa kati wa Leicester City na England, James Maddison. Lakini, inadaiwa kuwa Arsenal wanasita kulipa pauni milioni 60, malipo yanayotakikana kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(football.london)***

### LUKAKU NJIA MOJA
INTER Milan watakubali kwa shingo upande dau la takriban pauni milioni 100 kutoka Chelsea, ili kumwachia Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28 ***(Metro)***

### LAPORTE AITAKA LALIGA
MLINZI wa Hispania, Aymeric Laporte ameieleza wazi Manchester City kwamba anahitaji kuhamia katika Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu, huku Barcelona na Real Madrid zikiwa makini kumwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(90min)***

### DANILIUS SOKONI
KLABU ya Southampton na West Ham zinamtaka mlinzi wa kikosi cha vijana wenye umri wa miaka 21 wa Nice na Austria, Flavius Daniliuc mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail)***

### DANJUMA ANUKIA LIVERPOOL
LIVERPOOL inawaniwa kumsajili mshambuliaji wa Bournemouth, Arnaut Danjuma mwenye umri wa miaka 24, ambaye thamani yake ni pauni milioni 21.5. ***(Marca)***

### VILLA YAMTAKA ABRAHAM
KLABU ya Aston Villa ina matumaini ya kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na England, Tammy Abraham (23), na mlinzi wa Manchester United, Axel Tuanzebe. Wote walicheza kwa mkataba wa mkopo hapo Villa Park na waliisaidia klabu hiyo kupandishwa daraja na kuingia Ligi Kuu msimu wa 2018-19. ***(Telegraph)***

### KENEDY AGEUKA CHAMBO
CHELSEA wamemtoa kama ofa kwa winga Mbrazili, Kenedy kwa klabu ya Sevilla ikiwa ni kama sehemu ya mabadilishano ya kumsajili Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22. ***(Sun)***

### RONALDO AITAJA MADRID
CRISTIANO Ronaldo atataka kuondoka Juventus kuelekea Real Madrid, lakini mchezaji huyo anafahamu fursa ya kurejea pale Santiago Bernabeu zinategemea iwapo klabu hiyo ya Hispania itafanikiwa katika harakati zake za kumtaka mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22. ***(AS)***

### BRENTFORD YAJIONGEZA
KLABU ya Brentford ambayo imepanda kwenye Ligi Kuu England itakamilisha mkataba kwa kiungo wa kati wa Midtjylland, Jens Cajuste mwenye umri wa miaka 21, ambaye amehusishwa na taarifa za kuhamia Rennes. ***(Sportbladet)***

### LANG ANUKIA LEEDS
LEEDS United wanataka kumsajili mchezaji wa kikosi cha vijana walio chini ya umri wa miaka 21 cha Uholanzi, Noa Lang. ***(El Desmarque)***

-

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SPURS YAONGEZA THAMANI YA KANE

●●●Bosi wa timu hiyo azitaka klabu zinazohitaji huduma ya straika huyo kuwasilisha ofa...

**LONDON, ENGLAND**

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy ameweka wazi klabu yoyote itakayomtaka mshambuliaji wake, Harry Kane itatakiwa kutoa kiasi cha pauni milioni 160.

Imethibitika kuwa Kane hakurejea mazoezini na kikosi cha Spurs mwanzoni mwa wiki hii kama alivyopaswa kufanya, hii inadaiwa ni njia ya mchezaji huyo kujaribu kulazimisha usajili wake (kwenda Manchester City).

Inasemekana Kane anaamini alikuwa na makubaliano na Spurs kuwa ataruhusiwa kuondoka klabuni hapo kwenye dirisha hili la usajili huku City na Manchester United zikihusishwa na usajili wake.

Ripoti za sasa zinasema Levy ameweka thamani ya pauni milioni 160 kwa timu yeyote inayotaka kumsajili Kane.

Ingawa Kane alinukuliwa (msimu uliopita kabla ya Euro 2020) akisema hadhani kama anathamani ya pauni milioni 150 baada ya kuona Levy anavyoweka mazingira ya usajili wake kuwa mgumu.

Kwa upande wa City, wamejipanga kutoa zaidi ya pauni milioni 120 kwa Kane ikizingatiwa kuwa ana umri wa miaka 28 kwa sasa.

Kwa dau la City, likilinganishwa na kiwango cha Spurs - uhalisia ni City wanapungufu ya pauni milioni 40, kama wanataka kumsajili Kane.

Anayefaidika na hali hii kwa namna moja au nyingine ni United ingawa wanahitaji kumsajili mshambuliaji na wameamua kusubiri hadi msimu wa 2022/23.

Hapa ndio United wataingia sokoni kutafuta mrithi wa Edinson Cavani ambaye atakuwa amemaliza mkataba wake ndani ya Old Trafford.

Kwa hesabu za United, wanaamini muda kama huu mwakani Kane na Erling Haaland, wote watakuwa sokoni.

## HABARI MICHEZO

# MTIBWA SUGAR YAJITOSA KUMWANIA NYOTA YANGA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mtibwa Sugar umeonyesha nia ya kutaka kumsajili beki wa kulia wa Yanga, Said Makapu kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA.

Makapu pia ana uwezo wa kucheza kwa ufasaha nafasi ya kiungo mkabaji, beki ya kati na kulia, amekuwa hana namba kwenye kikosi cha kwanza cha Yanga.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Mohammed Badru alisema katika ripoti amependekeza nafasi za wachezaji anaotaka wasajiliwe, pia alitaja majina ya nyota anaowahitaji kama watapatikana.

Hata hivyo Badru hakuwa tayari kusema kama wameshaanza mazungumzo na Makapu.

Badru alisema anahitaji kusajili wachezaji wenye uzoefu na uwezo wa kukabiliana na ushindani uliopo katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na hataki kuona kikosi chake kinakuwa wasindikizaji.

Kocha huyo alisema hawezi kuweka wazi majina ya wachezaji wengine kwa sababu kuna wengine wanawindwa na timu nyingine, hivyo zinaweza kuongeza ushindani.

"Kuna wachezaji nimewataja majina, kwa sasa siwezi kuweka wazi majina hayo, ila tusubiri viongozi wafanyie kazi ripoti yangu kama nilivyopendekeza, ninahitaji beki wa kuli, beki wa kati na kiungo mkabaji," alisema Badru.

Aliongeza msimu uliopita walimaliza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa presha, hivyo wanajipanga kujiimarisha kwa kufanya usajili makini, ili makosa yaliyojitokeza yasijirudie.

"Hatutaki kujiweka katika presha kubwa kama ilivyokuwa msimu uliopita, hatutaki kurudia makosa yale yale, tumejipanga kufanya vizuri katika michezo yote ya ligi na Kombe la FA," Badru alisema.

Aliongeza anafahamu kila timu iko kwenye mchakato wa kuimarisha kikosi chake na wao wanahitaji kukamilisha malengo yao mapema na kuanza maandalizi ya msimu mpya kama walivyopanga.

"Ni kweli Makapu ni miongoni mwa wachezaji walioorodheshwa katika ripoti ya Kocha Bandru, kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu yetu kwa msimu mpya wa Ligi Kuu, tunafanyia kazi kuona kama tutampata maana kuna ofa kutoka timu nyingine zinamhitaji," kilisema chanzo chetu.




Mratibu wa mbio za Rock City, Kasara Naftal (kulia) akipokea mfano wa hundi yenye thamani Sh. milioni 20, kutoka kwa Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Mahusiano Benki ya KCB Tanzania, Christina Manyenye, kwa ajili ya maandalizi ya mbio hizo zitakazofanyika Oktoba 24, mwaka huu Jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Golikipa Azam apelekwa Namungo

**Na Adam Fungamwango**

AZAM FC, imesema imemtoa kwa mkopo golikipa wake, David Kisu kuelekea Namungo kwa ajili ya kuitumikia klabu hiyo katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema uamuzi huo umefikiwa baada ya kupokea maombi kutoka kwa mabosi wa Namungo na wao wakaridhia.

Popat alisema, wakati wakiruhusu Kisu kuondoka, klabu hiyo imemsajili kipa mpya, Ahmed Ali Suleiman kutoka KMKM.

"Tumemsajili kwa mkataba wa miaka miwili. Kocha wetu wa makipa, Idd Aboubakar alimhitaji kipa huyu. Na tangu msimu uliopita ilikuwa tumsajili, lakini alikuwa bado anasoma," alisema Popat.

"Kisu ataelekea Namungo kwa mkopo kwa sababu tumepata maombi na sisi tumeridhia, hivyo tutabaki na magolikipa watatu."

Kiongozi huyo alisema mchakato wa usajili kwao umefikia kiwango cha asilimia 90 na uamuzi wa kutoa wachezaji kwa mkopo unasaidia kukuza vipaji vya nyota husika na baadaye huwarejesha kwenye kikosi cha kwanza.

Msimu uliopita iliwatoa Oscar Masai ambaye alikuwa akiichezea Ihefu, Idd Kipwagile aliyepelekwa Namungo FC, Lusajo Mwaikenda, Masudi Abdallah na Paul Peter ambao waliichezea KMC, lakini, kwa sasa wamerudishwa na wataichezea timu hiyo kwenye michuano ya Kombe la Kagame.

# KCB, Rock City Marathon safi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya KCB Tanzania imekabidhi hundi ya Sh. milioni 20 kwa waandaaji wa mbio za Rock City Marathon zinazotarajiwa kufanyika Oktoba 24, mwaka huu Jijini Mwanza.

Akikabidhi hundi hiyo, Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Mahusiano KCB Tanzania, Christina Manyenye alisema udhamini huo unalenga kuunga mkono jitihada za waandaji wa mbio hizo, pamoja na serikali kwa ujumla katika kuhamasisha michezo na utalii wa ndani hapa nchini.

"KCB tunafuraha kwa mara nyingine kushiriki kikamilifu kwenye mbio hizi. Tumekuwa tukiguswa sana na masuala ya kimichezo sababu tunaamini ustawi wa sekta yetu ya benki unategemea sana uimara wa wananachi katika kujenga uchumi wao na ili hilo lifanikiwe, tunahitaji kuwa na watu wenye utimamu kiafya na kiakili. Michezo ni moja ya namna bora kabisa katika kujenga afya ya wateja wetu na kuburudika," alisema Manyenye.

Alisema, ili kutangaza utalii wa ndani benki hiyo itaendelea kushirikiana na waandaaji wa mbio hizo kuhakikisha zinafanikiwa kuvutia zaidi washiriki kutoka ndani na nje ya nchi, ambao ujio wao hautaishia katika kuimarisha sekta ya utalii pekee, bali utafungua milango ya mahusiano ya kibiashara kwa wakazi wa Jiji hilo.

Mratibu wa mbio hizo, Kasara Naftal aliishukuru benki hiyo kwa kuunga mkono mbio hizo.

"Ushiriki wa benki ya KCB iliyojijengea heshima kubwa kupitia huduma zake ndani na nje ya mipaka ya nchi utatusaidia pia kuvutia wadau na washiriki kutoka nje ya nchi, hatua ambayo ni muhimu katika kufanikisha agenda yetu ya kutangaza utalii wa ndani husani kanda ya Ziwa," alisema Naftal.

Alisema maandalizi ya mbio hizo yanaendelea vizuri huku akibainisha kuwa ubora wa vifaa kwa ajili ya washiriki wa mbio za mwaka huu ikiwamo medali na fulana unatarajiwa kuwa kivutio kikubwa kwa washiriki.

"Zaidi tunashukuru kuona viongozi mbalimbali wa kiserikali pamoja na wadhamini na wadau wetu wengine watashiriki kikamilifu kwenye mbio hizi." alisema mratibu huyo.

Naye, Afisa Biashara, Mahusiano ya Makampuni kutoka Tigo Pesa, Amani Chuo alisema kampuni hiyo imejipanga kikamilifu kuhakikisha washiriki wa mbio hizo wanajisajili kwa urahisi na kwa uhakika.

Wadhamini wengine wa mbio hizo ni pamoja na Kampuni ya TIPER, Pepsi, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB),Kampuni ya Uhandisi ya Magare, Unilever, NSSF, Hospitali ya Bugando, Hospitali ya CF, Garda World, Maji ya Uhai, Azam TV, Rock City Mall, Hotel Farm, EF Outdoor, The Cask na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) cha Jijini Mwanza.

# Michezo

Alhamisi Agosti 5, 2021

Nipashe




SPURS YAONGEZA THAMANI YA KANE HABARI UK 22



Kiungo wa Azam FC, Iddi Kipagwile, akiruka juu kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa KCCA ya Uganda katika mechi ya Kundi B ya mashindano ya Kombe la Kagame iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex Jumapili usiku. Azam ilishinda mabao 2-0 katika mchezo huo na leo itawakaribisha Messager Ngozi ya Burundi katika michuano hiyo. PICHA: MTANDAO

# LIGI KUU BARA SEPT. 29

**Na Mwandishi Wetu**

### Bodi ya Ligi yafunguka viporo sasa itakuwa historia katika msimu ujao...

MSIMU mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa mwaka 2021/22 ambao utashirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini umepangwa kufanyika kuanzia Septemba 29, mwaka huu imefahamika.

Simba ya jijini Dar es Salaam ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo, ikishinda taji hilo kwa misimu minne mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania, Almasi Kasongo, alisema Ligi Kuu itaanza rasmi baada ya mchezo wa Ngao ya Hisani utakaochezwa ifikapo Septemba 25, mwaka huu kwa kuwakutanisha watani wa jadi, Simba na Yanga.

Kasongo alisema mechi hiyo ya Ngao ya Hisani itachezwa kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na wanazitaka timu husika kujiandaa vyema kwa sababu wanafahamu mchezo huo unavuta hisia za wadau mbalimbali wa soka kutoka ndani na nchi jirani ya Tanzania.

Alisema ratiba kamili ya msimu mpya itatolewa hivi karibuni na itakuwa iliyokamilika ili timu ziweze kufanya maandalizi na kujiweka tayari na msimu huo mpya.

Kiongozi huyo alisema wanatarajia msimu mpya hautakuwa na mechi za viporo kwa sababu timu zote zitakuwa zinacheza kila raundi kwa wakati mmoja na kwa kufanya hivyo, ushindani uliokusudiwa kwenye ligi hiyo ya juu nchini utaonekana.

"Ligi yetu rasmi tutaifungua rasmi Septemba 25, ni mazingatio yetu na mwelekeo wetu kuwa na viporo sifuri, tusiwe na viporo kabisa, baada ya majadiliano marefu, mazungumzo sahihi, kwa kauli moja tumekubaliana na vilabu, ligi itakuwa inasisimama pale klabu nyingine zitakazokuwa na mechi za kimataifa," alisema Kasongo.

Aliongeza uamuzi huo umepata baraka kutoka kwa klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu na msingi huu umefikiwa baada ya kufahamu msimu ujao Tanzania itawakilishwa na timu nne katika mashindano ya kimataifa yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Alisema pia katika kikao cha pamoja na vilabu, wamefanyia maboresho kanuni ikiwamo kupata uwakilishi wa timu pale nchi inapopata nafasi nyingi kwenye michuano ya kimataifa na maboresho ya viwanja vitakavyotumika.

"Pia tumeziangalia kanuni ambazo zitasimamia yale yasiyopendeza, tuwe na ligi yenye weledi na adhabu kulingana na makosa yanayojirudia," Kasongo alisema.

Alieleza pia msimu ujao, timu zitakuwa zinapumzika siku tatu baada ya kutoka kwenye michezo ya kimataifa badala ya sita kama ilivyokuwa katika msimu uliopita na kwa kuzingatia hivyo, kalenda yetu itakwenda vizuri.

Timu zitakazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao ni pamoja na mabingwa Simba, Yanga, Azam FC, Biashara United, KMC FC, Tanzania Prisons, Kagera Sugar, Mtibwa Sugar, Ruvu Shooting, Polisi Tanzania, Dodoma Jiji, Namungo FC, Mbeya City, Coastal Union, Geita Gold FC na Mbeya Kwanza.

## SIMBA: MIQUISSONE ATAZALISHA VISHINDO

**Na Saada Akida**

KOCHA na mchezaji wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Talib Hilal, ameutaka uongozi wa klabu hiyo kumruhusu nyota wake, Luis Miquissone kujiunga na Al Ahly ya Misri kwa sababu ya dau nono la Dola za Marekani 900,000 ambazo wameweka mezani.

Tayari Simba imemtambulisha kiungo mpya, Peter Banda aliyesaini mkataba wa miaka mitatu na kutajwa huenda akawa ni mrithi wa Miquissone.

Talib alisema dau hilo ni kubwa na Simba inatakiwa kufahamu mpira ni pesa na ofa hiyo iliyotolewa na mabingwa hao wa Afrika ni nzuri na inaweza kusaidia kununua wachezaji wengine watatu wazuri kutoka nje ya Tanzania.

Alisema sasa ni wakati wa Simba kuwa makini kufanya biashara kwa sababu ana imani kwamba nyota huyo atawafungulia milango wengine na kuhakikisha wanapopata fedha hizo wanasajili wachezaji wengine watakaoziba mapengo mapema.

"Simba hawana sababu ya kuchelewesha ofa hiyo kwa kuangalia faida kwa klabu, pia nzuri hata kwa mchezaji mwenyewe kujaribu bahati yake kwingine, mbona TP Mazembe walimuuza Mbwana Samata na alikua ndio mfungaji wao pekee,".

"Usajili wa Peter Banda kwangu ni mchezaji mzuri na ndio mrithi sahihi wa Miquissone, ana uwezo na kiwango cha kucheza vizuri na ataisaidia Simba kufikia malengo yake," alisema Talib.

Naye Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, alisema wataweka wazi baada ya mchakato wa usajili wa Miquissone utakapokamilika kwa sababu bado uamuzi wa kuondoka au kubakia Simba haujakamilika.

"Tumewekeza zaidi kwa upande wa wachezaji ili kuwa na kikosi bora, mashabiki wawe na subira, mambo mazuri yataonekana katika eneo hilo kwa kupata wachezaji bora kulingana na mapungufu yetu ambayo yalionekana msimu uliomalizika, tutakuwa na kishindo," alisema Mangungu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002